Chakula Cha Kiroho Kwa Wakati Wake

Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini.

Vipi, sasa huo namna hii:

Sasa naamini, sasa naamini,
Yote yatendeka, sasa naamini;
Sasa naamini, sasa naamini,
Yote yatendeka, sasa naamini.

Na tuendelee kusimama sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

Bwana, jalia huu usiwe ni wimbo tu, lakini iwe ni vilindi kabisa vya moyo wetu vikiimba, "Sasa naamini!" Wanafunzi walisema wakati mmoja, baada ya Yesu kwisha kufanya kazi nyingi sana kuu, walisema, "Bwana, sasa tunaamini."

Yesu akasema, "Je! mnasadiki sasa?"

2 Wakasema, "Tunaamini kwamba Wewe wafahamu mambo yote wala huna haja ya mtu akufundishe." Kwa hiyo, Baba, usiku wa leo tunatambua ya kwamba Wewe huhitaji mafundisho yetu, bali sisi tunahitaji Yako. Kwa hiyo tunaomba kwamba Wewe utatufundisha jinsi ya kuomba, jinsi ya kuishi, na jinsi ya kuamini. Tujalie, Bwana, katika ibada hii usiku wa leo. Kama tunapungukiwa na cho chote, tupe, Bwana. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

3 Ninajua wengi wenu wanasimama tena usiku wa leo. Na, huko nje, nilikutana na makundi yaliyosema yasingeweza kuingia, nao wanasikiliza redio zao katika motokaa mbalimbali. Na sasa tutajaribu kuharakisha upesi tuwezavyo usiku wa leo, Jumapili usiku, tumeutoa kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa, tufanye mstari wa maombi kwa kuwa tunaweza kuufanya mmoja hapa. Lakini tunaiweka wakfu ibada hii usiku wa leo kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa.

4 Nami nawatakeni mjengeke sasa katika. . .Haya Mausia Matakatifu ya Mungu, katika Imani ile, Imani ya saa hii. Imani! Itahitaji imani zaidi kuliko ilivyopata kuwa katika wakati wo wote, kwa maana hii haina budi kuwa ni imani ya kunyakuliwa, kutwaliwa juu. Na kwa hiyo tunawatakeni mwamini usiku wa leo yote mliyoona, mliyosikia, Neno mlilosikia likihubiriwa, i— ishara na maajabu mliyoona yakifanywa. Tunataka mkusanye hayo yote katika moyo wenu, na kuyatafakari, iwapo hayo ni Mungu ama siye.

5 Ni kama Elisha wa kale, aliyesema, "Kama Mungu ni Mungu, basi mtumikieni." Na kama Yesu ndiye kiini cha kila kitu kwa Mkristo, basi nafikiri tunapaswa kuachilia kila kitu kingine na kumshikilia Yeye. Kumbukeni, Yeye ndiye Kiini, Yeye ni Nyota ya Kaskazini, Yeye ni Mkataa, Yeye ni Yakini. Na iwapo Yeye ndiye Nyota ya Kaskazini . . . Kuna kitu kimoja tu ambacho kitaelekeza kwenye nyota ya kaskazini, hicho ni dira yako unayoabiri nayo. Nayo Dira ninayojaribu kuabiri nayo ni Neno, nalo Neno daima huelekeza Kwake.

6 Basi tunajisikia kama kwamba tunapitia katika wakati mkuu wa dhiki na majaribu, mshangao wa wakati na dhiki kati ya mataifa, na mambo ya kila namna yanayotendeka, na wakati mwingine kana kwamba ninamezwa . . . Kila mahali ninakoangalia, ni kama kwenye ninii—kwenye meli baharini. Nami nimekabidhiwa Meli hiyo. Basi tutafikaje? Na hapa laja wimbi moja leupe, kubwa mara mia kadha kuliko meli yangu. Lakini tutayavuka, kila moja. "Sisi ni zaidi ya washindi kwa Yeye." Kapiteni, Kapiteni Mkuu, ameshika kamba upande mmoja wa mwisho wa meli, Yeye ataivuta ivuke. Tutavuka kila moja ya hayo.

7 Sasa, usiku wa leo, ili kwamba tuweze kuharakisha na kuwaacha mtoke mapema. Tunathamini kuendesha kwenu magari kutoka mbali, na kadhalika, na jinsi inavyowabidi kuendesha, na kujitolea kunakowabidi kujitolea. Na, mnaona, hilo linanifanya nifikie mahali ambapo ningetaka tu kusimama na kuendelea tu kuzungumza na kufanya yote niwezayo kuwasaidia. Lakini ninapokuwa hapa ninajaribu kusukumiza ndani kila kitu niwezacho, ili kusaidia katika wakati ambapo tupo hapa sasa. Halafu uchukue . . . Kama ukiwapa watu mengi kupita kiasi kwa wakati mmoja hawawezi kuyakumbuka. Ina—inakupasa tu kuchukua kitu kimoja na kudumu nacho kwa ajili ya mtu huyo mpaka waone jambo hilo. Na basi watakapokuwa wameshikilia hilo moyoni mwao, basi wao wataninii . . . ndipo uwafundishe jambo lingine. Hatua kwa hatua tu tunapoendelea.

8 Sasa, ninyi ombeni na mwe hodari, na mwamini sasa usiku wa leo kwa ajili ya kuponywa. Sidhani kuna swali lo lote mioyoni mwenu kuhusu wakati tunaoishi. Siamini kuna swali lo lote mioyoni mwenu kuhusu kama Mungu yuko katikati ya watu Wake ama hayuko. Ninaamini nyote mnaamini jambo hilo. Nami . . . Sina shaka moyoni mwangu kuhusu jambo hilo. Nami na—na—najua watu wangu, rafiki zangu, marafiki wa Kristo, watoto wa—wa Kristo, wanaamini jambo hilo.

9 Na linanipa furaha kuu kupata kuona wakati unapojua ya kwamba una Ujumbe unaotoka kwa Mungu, nawe unautoa kwa watu na kuona watu wanaupokea Huo. Ndipo unaangalia nyuma na kusema, "Asante, Baba." Loo, ni furaha jinsi gani basi kuona watoto wakila Chakula walichopelekewa! Je! mnatambua hilo lilikuwa ni ono miaka kadha iliyopita, papa hapa Maskanini hii?

Ni kweli, "Chakula cha Uzima." Ndugu Neville, unakumbuka jambo hilo, huenda unakumbuka. Wakati mkuu sana!

10 Sasa hebu tufungue, kama mnataka kufuatilia somo ama kuliandika, ninii tu. . . Siamini ingekuwa vema kufanya ibada bila kusoma Neno la Mungu na kutoa maelezo kidogo, kama itakuwa ni ibada ya kuponya ama ya namna yo yote. Sote tunafahamu. Hakuna wageni kati yetu, nadhani. Lakini sote tunafahamu kuponya ni nini. Si kitu ambacho mtu fulani anakutendea; ni kile ambacho Mungu tayari amekwisha kukutendea. Wokovu ni vile vile. Kitu tu, ni, kuwafanya watu waamini jambo hilo ni la Kweli. Na Mungu analifundisha katika Neno Lake na halafu anawathibitishia wale watakaoamini Hilo, kwa maana Yeye alisema, "Yote yawezekana kwaa waaminio."

11 Unasema, "Hakuna kisichowezekana kwa Mungu." Unaamini jambo hilo? Hakuna kisichowezekana kwako, pia. "Kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao," (Mungu ni Mtu mmoja) "kwao waaminio." Mnaona? Kwa hiyo hakuna kitu kisichowezekana kwako, kwa ajili yako, kama wewe unaweza tu kuamini.

12 Sasa katika Wafalme wa Kwanza, sura ya 17, ninataka kusoma aya saba za kwanza, Bwana akipenda.

> *Basi Eliya Mtishibi, wa wageni wa Gileadi, akamwabia Ahabu, Kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake, hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, ila kwa neno langu.*
>
> *Neno la Bwana likamjia, kusema,*
>
> *Ondoka hapa, geuka, uende upande wa mashariki, ujifiche karibu na kijito cha Kerithi kinachokabili Yordani.*
>
> *Itakuwa, utakunywa maji ya kile kijito; nami nimewaamuru kunguru wakulishe huko.*

Angalieni, "wakulishe huko," si mahali pengine. "Huko!"

> *Basi akaenda akafanya kama BWANA,* ama *alivyosema BWANA; kwa kuwa akaenda akakaa karibu na kijito cha Kerithi, kinachokabili Yordani.*
>
> *Kunguru wakamletea mkate na nyama asubuhi, na mkate na nyama jioni, akanywa maji ya kile kijito.*
>
> *Ikawa, baada ya siku kupita, kile kijito kikakauka, kwa sababu mvua haikunya katika nchi.*

13 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusoma Neno Lake. Na sasa, usiku wa leo, ninataka kuchukua somo kutoka hapo, liitwalo, "Chakula cha kiroho kwa wakati Wake." Asubuhi ya leo tulikuwa na—na somo juu ya—juu ya "Kumtendea Mungu kazi, ama kujaribu kumfanyia Yeye huduma bila ya kuwa. . . ukiwa

nje ya wakati wake, majira, mahali, ama mtu.” Na sasa hili ni: *Chakula Cha Kiroho Kwa Wakati Wake.*

14 Nabii huyu, Eliya, tunajua machache sana juu yake. Lakini tunajua ya kwamba yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu, pia alikuwa mtumishi wa Mungu kwa saa ile.

15 Naye Mungu ametumia Roho Wake ambaye alikuwa juu ya Eliya, tayari mara tatu, naye anaahidi mara mbili zaidi; mara tano, kwa ajili ya neema. Yeye alimtumia juu ya Eliya; akaja juu ya Elisha katika sehemu maradufu; akawa juu ya Yohana Mbatizaji; na inatazamiwa kuja kumkaribisha tu Bibi-arusi wa Kimataifa; halafu aje pamoja na Musa kuwapeleka Wayahudi nyumbani. Hiyo ni kweli. Mara tano kwamba Mungu ameahidi kuitumia Roho ya Eliya, na tayari amefanya hivyo mara tatu.

16 Sasa, nabii huyu mkuu, hatujui alikotoka. Tunajua alikuwa Mtishibi. Lakini jinsi alivyokuja . . .

17 Tunajua machache juu ya manabii. Hatujui wanakotoka. Mara chache sana . . . Kama vile, sijui juu ya ye yote aliyetokea kwenye kanisa ama aliyetokana na ukoo fulani. Ilikuwa ni mtu tu wa kawaida ambaye alikuwa haogopi, na, mara nyingi, hana elimu. Nao hawakuandika cho chote kamwe, wao wenyewe. Isaya na Yeremia, wachache wao, waliandika kidogo, lakini mtu huyu mkuu Eliya hakuandika hata kitu kimoja. Wengi wao hawakuandika; labda hawangeweza kuandika. Lakini walikuwa ni watu shupavu. Hakuna mtu katika Biblia aliye kama hao manabii wa kale. Waliasi falme, wafalme, watu, makanisa, na kila kitu kingine, na kusimama imara juu ya Neno la Mungu, naye Mungu akawathibitisha kuwa wao ndio sahihi. Walikuwa shupavu sana.

18 Naye huyu Eliya alikuwa mmoja wa shupavu sana kuliko wote. Alikuwa mtu wa nyikani. Alitokea nyikani; aliishi nyikani. Biblia ilisema alivaa . . . alikuwa mwenye nywele nyingi, na alivaa ngozi ya kondoo, na kipande cha ngozi, ya ngamia amejifunga viunoni mwake, ninii sana . . . sharafa zimejaa usoni, nami naweza kuwazia alikuwa shupavu sana, vile alivyoonekana.

19 Lakini hatukuninii . . . wao wote hawakufa. Wote—wote hawajafa. Katika siku za Baraza la Nikea . . . wengi wenu watu mliosoma *Baraza la Nikea la Kanisa la Mwanzoni*, wakati wao walipotaka kufanya madhehebu kutoka kwake na kuyavunjilia mbali makanisa mengine yote, na wajikusanye kwenye moja, walipolifanya hilo Baraza la Nikea, watu shupavu kama Elisha wakaja pale kutoka nyikani, wakila mboga peke yake; watu shupavu na wakuu. Lakini wale wakuu, wale waheshimiwa, chini ya Konstantino, na kadhalika, walinyamazisha sauti yao. Kwa sababu hao, wakiwa manabii, walijua ya kwamba punje ya ngano ya Kanisa Bibi-arusi ilipaswa kuanguka ardhini, kama

vile punje ya ngano katika Bwana Arusi ilivyopaswa kuanguka ardhini. Na hapo ikalala kwa miaka elfu moja.

20 Hiyo ndiyo sababu wao wanaandika katika vitabu siku hizi, "Yuko wapi huyo Mungu aliye kimya ambaye angesimama na kuangalia, aone watoto wadogo wakiuawa, na wanawake wakiraruliwa vipande-vipande na simba, Naye anaketi huko mbinguni wala hasemi neno juu ya jambo hilo?" Wao hawajui Neno. Hiyo punje ya ngano haina budi kuanguka ardhini. Mungu mwenye haki angewezaje kusimama na kumwangalia Mwanawe Mwenyewe akifa na kutemewa mate, na kadhalika? Lakini ni kulingana na Neno, haina budi kuwa hivyo. Na hivyo ndivyo ilivyo hata kwenye saa hii.

21 Mtu huyu, yeye alikuwa ni mtu mashuhuri. Alikuwa na kizazi chenye dhambi mbele yake. Ahabu alikuwa mfalme, babaye aliyemtangulia alikuwa mwovu. Tangu wakati wa Sulemani, kumekuwako na mfalme mmoja mwovu baada ya mwingine. Naye mtu huyu, Ahabu, aliyetawala miaka ishiri na miwili katika Samaria, alikuwa ndiye mbaya sana kuliko wote. Yeye alikuwa ni wa kisasa kwelikweli. Aliamini katika dini, bila shaka. Naye alifanya kila kitu katika mwelekeo wa kisasa. Alikuwa na manabii wake mwenyewe mia nne wa Kiebrania, wote wemesoma vizuri na kufunzwa. Mungu alimtumia mmoja na wala yeye hangeamini, na huyo alikuwa ni Eliya.

22 Lakini Eliya, huyu Mtishibi, alikuwa ni mtu wa nyikani. Si mtu wa mchezo; alikuwa mtu mkali. Basi siku moja, baada ya Ahabu kutenda dhambi mpaka Mungu hakuweza kuvumilia jambo hilo tena, Yeye alinena na Eliya nyikani. Ndipo huyu hapa anashuka kwenda zake Samaria, kama nilivyoelezea mara nyingi; labda hizo sharafa nyeupe zikitokeza usoni mwake, kichwa chenye upara kiking'aa juani, macho madogo membamba ya kizee, huko nyuma ameshika fimbo mkononi mwake, tabasamu usoni mwake, alienda moja kwa moja mpaka kwa mfalme wa Israeli, na kusema, "Ninii . . . Hata umande hautaanguka mpaka nitakapouita."

23 Mungu na atupe mtu kama huyo, mnaona, mtu anayejua wanavyofanya na BWANA ASEMA HIVI.

24 Sasa, tunaona ya kwamba kabla yeye hajafanya jambo hili, ambalo Mungu alikuwa amemwitia. Mungu alikuwa amezungumza naye na, kwa hiyo, yeye hakuogopa kitu. Hakuonea shaka ujumbe wake, usingetimia; alijua ungetimia! Alijua ulikuwa ni kulingana na Neno la Bwana, na alijua yeye alikuwa ni nabii wa Mungu kwa ajili ya saa hiyo. Kwa hiyo haidhuru kama mfalme angemkata kichwa, amtupe gerezani, kitu cho chote kile wangelifanya, haikubadilisha cho chote kwake; yeye alikuwa na agizo, "BWANA ASEMA HIVI," ya kusema papo hapo usoni pa mfalme. Ni mtu shupavu jinsi

gani! Lakini kabla ya kufanya jambo hili, kutabiri huu ukame mkubwa . . .

25 Kwa kuwa Mungu hataachilia dhambi itendeke bila ya kuihukumu. Lazima kuwe na hukumu. Sheria ina faida gani bila—bila hukumu? Ingefaa nini, kusema, "si halali kuwasha taa," wala hakuna faini nyuma yake, ama hukumu nyuma yake? Haingekuwa ni sheria. Kwa hiyo kuna hukumu ya dhambi. Na wakati Mungu anapofanya sheria, na hiyo sheria— sheria inavunjwa, basi lazima pawe na hukumu kwa ajili yake.

26 Na taifa hili lilikwisha asi sheria Zake zote. Loo! wao walikuwa na kanisa kubwa, walikuwa na hekalu. Walikuwa na watu wengi wenye elimu. Walikuwa na manabii nchi nzima, walikuwa na shule zao hao, zikiwatoa kama vile mitambo. Basi walikuwa na manabii wengi sana, walikuwa na makuhani we—wengi, walikuwa na waandishi wengi, na walikuwa na dini tele, bali walikuwa wameliacha Neno la Mungu. Kwa hiyo Mungu akaita mtu ambaye si wa vyeo vyao kabisa, na akamtuma akiwa na BWANA ASEMA HIVI.

27 Basi angalia jinsi Yeye anavyowashughulikia walio Wake. Kabla ya Yeye kumtuma nabii huyu na ujumbe, Yeye alisema, "Eliya, shuka uende ukamwambie Mfalme Ahabu mambo haya. Na sasa, utakapofanya jambo hilo, ondoka kwake upesi sana, kwa maana nimekutengenezea mahali utakapoenda wakati wa ukame. Nitakutunza, Eliya, kama ukihubiri tu Neno Langu, ukifanya tu nitakayokwambia ufanye."

28 Sasa naenda kuifananisha huduma hii kuu, usiku wa leo, ya Eliya na ule wakati wa Eliya, na saa tunayoishi sasa. Ninaamini vinafanana kabisa. Ninawazia juu ya mataifa . . . kama mimi . . . tungalikuwa na wakati wa kurudi nyuma, lakini ninataka kutumia wakati mwingi sana katika mstari wa maombi.

29 Kwa hiyo kama tungaliweza kurudi nyuma na kuona, Israeli walikuwa wameitwaa Palestina katika msingi ule ule ambao sisi tumeitwaa Marekani. Sisi tuliingia Marekani hii na kuwafukuza wenyeji wake, ambao walikuwa ni Wahindi, na tukaimiliki nchi. Na vivyo hivyo Israeli nao waliingia Palestina, chini ya uongozi wa Yoshua, chini ya Mungu, na kuwafukuza wenyeji wake na kuitwaa nchi.

30 Na wafalme wao wa kwanza walikuwa ni watu wenye nguvu; Daudi, Sulemani, na watu wakuu. Marais wetu wa kwanza walikuwa watu wakuu: Washington, Lincoln, na kadhalika. Halafu hatimaye hao marais ama wafalme wakaanza kuharibika zaidi siku baada ya siku, na hatimaye wakaishia kwa huyu Ahabu. Mfano halisi, mfano unaofanana kabisa na siku zetu. Nao watu walikuwa wamekuwa wa kisasa sana hawakutaka kusikia Neno la Kweli la Bwana.

31 Nawe unaweza kuwazia, juu ya watu wa kisasa kama hao, vile mtumishi halisi wa Mungu angesikika kwao. "Mbona,

alikuwa ni mwenda wazimu, alikuwa amerukwa na akili. Isingewezekana kuwepo na kitu kama hicho." Wao walikuwa ni wa dini, watu wa dini sana. Walikuwa na mtu mwaminifu, walikuwa na watu waaminifu. Walikuwa wa dini sana.

32 Kwa hiyo yeye alijua kwamba kungehitajika zaidi ya theolojia ya kawaida, kungehitajika zaidi ya—zaidi ya ujumbe wo wote wa kawaida, kungehitajika zaidi ya kuhubiriwa tu kwa Neno, ili kuivunja mioyo yao ya mawe. Yeye alijua kulihitajika BWANA ASEMA HIVI kuleta hukumu ile juu ya watu wale, kwa hiyo alijua hilo wakati alipotoka na BWANA ASEMA HIVI. Na ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Kupuuza Hilo, ilikuwa ni hukumu. Tunaliona jambo hilo katika siku zetu, pia. Tunaliona jambo hilo katika siku yo yote. Hakuna kilichosalia ila hukumu unapovuka mstari wa rehema.

33 Sasa, mfano huo hapo ndio nitakaomfananisha Eliya nao, nitakaofananisha kanisa nao leo hii, kanisa la siku hizi. Kabla tu ya hukumu, yeye akapokea ujumbe huu. Eliya, yeye aliwakilisha, akitunzwa katika mambo ya kawaida, chakula chake cha kawaida, kwa sababu haingenyesha sasa, kulingana na Neno la Mungu, kwa miaka mitatu na miezi sita, ama mpaka Eliya alipoiagiza. "Wakati wo wote utakaotamka, Eliya, ndivyo itakavyokuwa." Kwa hiyo yeye akamwendea mfalme, na kusema, "Hakutakuwa hata na umande utakaoanguka mpaka nitakapouagiza." Hilo ni zi—zito kweli, sivyo? Huo ni ujumbe kweli!

34 Na sasa tutafananisha huo na ukame wa kiroho wa siku hizi. Sasa, sote tunajua, tunajua sana, kwamba kuna ukame mkubwa wa kiroho leo, tukinena kiroho. Na, mwajua, huo ulitabiriwa na manabii, kabla tu ya kule Kuja Mara ya Pili kwa Kristo, kasema, "Kutakuja njaa nchini, wala haitakuwa kwa ajili ya mkate tu, bali kwa ajili ya kulisikia Neno la Mungu." Na siku hiyo ni sasa, "kulisikia Neno la kweli la Mungu." Sasa, hii inafananisha ukame wa kawaida na wa kiroho.

35 Dhambi na kutokuamini, kwa waalimu wa uongo na watu wa kisasa kanisani, kulikuwa kumewafikisha kwenye kuja huku, kwenye hukumu ijayo. Halafu walikuwa wameliacha Neno la Mungu na nabii Wake, wakageukia kwenye mapatano ya kitheolojia ya Neno.

36 Mnaona hapa, ndio papo hapo kwenye wakati kama huo ambapo Mungu daima huinua jambo fulani. Maana, Yeye, daima, Yeye hatendi neno lo lote mpaka kwanza alifunue kwa watu, Naye daima hulifunua kwa njia ya watumishi Wake.

37 Sasa, lakini Eliya, katika wakati huu, alikuwa na mahali pa siri ambapo Mungu alikuwa amemchagulia kwenda. Hilo ndilo jambo tunalotaka kuona sasa kabla tu hatujafanya mstari wa maombi. Eliya alikuwa na mahali pa siri alipoandaliwa na Mungu Mwenyewe. Sasa, kanisa kamwe halikumwandalia

mahali hapo, mfalme kamwe hakumwandalia mahali hapo, yeye hakujiandalia mwenyewe, bali Mungu alimwandalia Eliya mahali pa siri apate kulishwa wakati wote kipindi cha ukame, mahali ambapo chakula chake kiliandaliwa siku baada ya siku. Haikumbidi kushangaa itakuwaje kesho ama kushangaa kama chakula kitaisha. Mungu alisema, "Nimewaamuru kunguru nao watakulisha." Ni jambo la ajabu jinsi gani, mfano wa mahali petu pa siri katika Kristo.

38 Wakati baraza la ulimwengu na yote yanayoendelea leo, linalosema, "Siku za miujiza zimepita." Zile nguvu kuu za Mungu zimeondolewa makanisani. Wanaonekana kama, tena, hawana kitu ila "shaba iliayo na upatu uvumao." Tunajua jambo hilo kuwa ni kweli. "Na mfano wa utauwa, na kukana Nguvu zake."

39 Ni jambo lile lile ambalo Daudi alifanya asubuhi ya leo, akiwa na magari ya maksai, wakaliacha Neno. Wakati Neno lilipoletwa na likakabidhiwa kwao, wao hawakulitaka; kwa hiyo, walikuwa wameliacha.

40 Hivyo ndivyo watu hawa walivyokuwa wamefanya katika siku za Eliya, waliliacha Neno. Walidhani walikuwa na Neno, bali hawakuwa Nalo. Kwa hiyo angalia basi katika . . .

41 Kwenye wakati ambapo Yeye alikuwa anaenda kuhukumu wasioamini, Yeye aliandaa njia kwa mwamini. Yeye hufanya jambo lile lile kila wakati. Katika siku ambapo Yeye alienda kuuharibu ulimwengu kwa maji, Yeye alimwandalia Nuhu njia ya kutokea. Katika siku ambazo alikuwa anaenda kuizamisha Misri, Yeye aliwafanyia watu Wake njia ya kutokea kupitia baharini. Jinsi Mungu anavyofanya njia Yake! Na mahali pasipo na njia, Yeye ndiye hiyo Njia. Yeye ndiye Njia hiyo!

42 Sasa tunatambua ya kwamba tunakabili baadhi ya ninii . . . moja ya masaa yaliyo muhimu sana ambayo historia imepata kujua. Si hasa bomu lenye kombola linalong'aa, lenye ncha kali mbele yake, ambalo tunapaswa kuogopa. Makanisa ndiyo tunayopaswa kuogopa. Saa tunayoishi ndiyo tunayopaswa kuangalia.

43 Sasa angalia, lakini Mungu alimtengenezea Eliya njia ya kutokea. Naye amewatengenezea watoto Wake waaminio njia ya kutorokea jambo hilo sasa, hasira na mambo yajayo.

44 Kwa sababu, Mungu asingekuwa mwenye haki kuwahukumu hao watu na kuwaletea hukumu, na kuizamisha Sodoma na Gomora, na kuuzamisha Kapernaumu katikati ya bahari, na kuvihukumu vizazi hivyo, na Sodoma na Gomora, halafu atuachilie tufanye jambo lile lile na eti sisi tuponyoke. Sisi tuna hakika tu ya hukumu kama walivyokuwa na hakika ya hukumu. Sasa tunaona ya kwamba ninii . . .

45 Wakati mambo haya yalipotokea, mtindo wa kisasa wa siku hizo, Mungu alimwinua mtu fulani katika siku hiyo,

ama alimwinua mtu, tuseme, kukabiliana na nguvu hizo, nao hawakumsikiliza. Walidhani alikuwa na kichaa, "Amerukwa na akili. Ati alikuwa tu mzee mshupavu fulani wa dini, mpumbavu aliyetokea jangwani, kwa namna fulani yeye ni juha la msituni." Lakini, hata hivyo, yeye alikuwa na Neno la Bwana.

46 "Neno halimaanishi linavyosema," wao eti wanasema siku hizi. "Loo, vema, Biblia ni kitabu cha historia." Nadhani wewe umeona jambo hili, ya kwamba sasa wao wanadai, ya kwamba, "Hawa hakula tofaa, yeye alikula . . . " Ilikuwa nini? Ninaamini . . . "Ilikuwa ni embe dodo," ndivyo wanavyosema leo. "Ilikuwa ni embe dodo." Halafu basi, ya kwamba, "Musa hakuwavusha kamwe wale wana kupitia Bahari ya Shamu. Ilikuwa ni msitu mkubwa wa matete, huko upande mwingine wa hiyo bahari, naye alipitia katika bahari ya matete." Basi ni vipi hayo maji, m—a—j—i, yalifanyaje ukuta pande zote mbili; wakapitia kwenye nchi kavu, basi? Loo, upuzi kama huo! Lakini, unaona, inahitaji siku ya namna hiyo kushusha hasira ya Mungu juu ya watu. Ndicho inachohitaji.

47 Wao husema hakuna kitu kama—kama hii . . . Hata watu wa kanisa hawaamini miujiza. "Nitakupa dola elfu moja," wao wakasema, "unionyeshe mwujiza. Nionyeshe mwujiza!" Vema, wao wasingeweza kuuona hata kama kungalitendeka mambo elfu mbele zao. Mbona, wao, wasingeweza kuona jambo hilo.

Unasema, "Hiyo haiwezekani." Loo, la, sivyo.

48 Eliya wakati mmoja alikuwa kule Dothani, nalo jeshi la Shamu lilikuwa limekuja likauzingira mji, ili wamchukue, kwa sababu wao walijua hapo ndipo ngu—nguvu za lile taifa zilipolala, zilikuwa ndani ya yule mwonaji. Mbona, mfalme . . . Mmoja wa hao watu alimwambia mfalme wa Shamu, akasema, "Ati, wajua, nabii Eliya, yule Mtishibi, humwambia mfalme wa Israeli maneno unenayo katika chumba chako cha siri."

49 Akasema, "Nendeni mkamkamate jamaa huyo! Huyo ndiye jamaa anayetuzuia." Ndipo jeshi lote la Shamu likapenya kisiri likauzingira Dothani. Walikuwa wameuzingira kabisa.

50 Basi Gehazi, m—mtumishi wa nabii, akaamka, naye akasema, "Ole wetu, baba yangu, majeshi yametuzingira kila mahali hapa. Tumezingirwa kabisa."

51 Akasema, "Mbona, kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao." Mnaona?

Ndipo Gehazi akaangalia kila mahali, akasema "Sioni mtu."

52 Yeye akasema, "Bwana Mungu, yafumbue macho ya kijana huyo." Ndipo macho yake yakafumbuka, na kumbe! vilima vyote vimejaa Malaika na magari yamesimama kila mahali, Jeshi lisiloonekana.

53 Eliya akatoka moja kwa moja akaenda kule nje, na Biblia ilisema, "Akawapiga kwa upofu." Akaondoka akawaendea;

wao walikuwa vipofu kwake. Akajitokeza na kusema, “Je! mnamtafuta Eliya?”

Yeye akasema, “Naam, tunamtafuta.”

54 Akasema, “Njoni, nitawaambia barabara mahali alipo,” naye akawaongoza moja kwa moja kwenye maoteo, moja kwa moja mahali ambapo yale majeshi yalitoka moja kwa moja yakaenda yakawanasa.

55 Sasa, Biblia ilisema, “Aliwapiga kwa upofu.” Hilo latosha. Na watu ni vipofu sana kiroho leo, hata Bwana Mungu aje katikati ya watu na kufanya jambo lo lote, na mambo aliyoahidi, wao bado hawawezi kuliona jambo Hilo. Wao ni vipofu kiroho; hawamjui Mungu, hawajui Uweza Wake mkuu. Sasa, tunaona ya kwamba wao walifanya jambo hilo katika siku za Eliya, nao hata sasa wanafanya hivyo leo. Mungu huwapiga kwa upofu. Wao wanasema leo, ya kwamba, “Hakuna miujiza, hakuna kitu kama hicho, yote haya ni sisimko la mwili.”

56 Nao walisema jambo lile lile juu ya Eliya, kwa sababu wakati alipotwaliwa juu naye Elisha akapachukua mahali pake, naye alikuwa ni kijana mwanamume, alipata upara akiwa kijana, watoto walitoka mbio wakimfuata nyuma yake, na kusema, “Ewe mzee upara, mbona hukunyakuliwa pamoja na Eliya?” Mnaona, wao hata hawakuamini jambo hilo hapo mwanzo, hao watu, baada ya mambo mengi sana kufanywa. Na mtu huyu mashuhuri wa Mungu alikuwa amehamishwa akaenda Mbinguni kwa gari la farasi wa moto, nao watu bado hawakuamini jambo Hilo. Na waliwaachilia watoto wao wamkimbilie mtu huyu nyuma na kusema, “Ewe mzee upara, mbona hukupaa juu?” Mnaona? Halafu basi nabii huyu akawalaani hao watoto, na dubu wa kike akawaua arobaini na wawili miongoni mwao.

57 Sasa angalia. Leo, kama ilivyokuwa wakati huo, wao waliweka fasiri yao wenyewe kwenye Neno. Sasa, kama wao wakitaka kufanya jambo hilo, hiyo ni juu yao, bali wao wanajaribu kutufanya tuamini jambo hilo. Biblia ilisema ya kwamba, “Neno hili la Mungu si la kujifasiria atakavyo mtu ye yote.” Mungu hujifasiria Mwenyewe. Mungu huthibitisha Neno Lake, na hiyo ndiyo fasiri Yake. Kama nilivyosema mara nyingi, Yeye alisema hapo mwanzo, “Iwe nuru,” na nuru ikawepo. Hilo halihitaji kufasiriwa; lilitukia. Alisema, “Bikira angepata mimba,” akapata. Alisema Yeye angemwaga “Roho Wake,” Naye akammwaga. Kisha akasema, “katika siku za mwisho,” mambo ambayo Yeye angefanya, Naye anayafanya! Halihitaji fasiri yo yote; Mungu anajifasiria Mwenyewe. Haidhuru mtu mjinga angesema nini, hilo halimzuii Mungu hata kidogo.

58 Wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alikabiliana na kutokuamini kwingi vile vile kama tulivyo nako leo, na labda zaidi. Lakini hilo halikumzuia; Yeye aliendelea tu kutenda kazi na kutekeleza shughuli Zake, huku Mungu akithibitisha

kila alilokuwa anatenda. Alisema, "Mimi si peke Yangu. Mimi na Baba Yangu ni mmoja; Yeye anaishi ndani Yangu. Si mimi ninayetenda kazi, ni Baba anayeishi ndani Yangu. Na kama nisipozitenda kazi Zake, basi msiniamini; lakini kama nikizitenda kazi hizo na hata hivyo ninyi hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi hizo." Mnaona? Kwa maneno mengine, wao . . . "Yachunguzeni Maandiko," Yeye alisema, "kwa kuwa humo ndimo mnamodhani mna Uzima wa Milele, ni kwa kuyajua Maandiko. Nayo Maandiko, Yenyewe, yananishuhudia Mimi." Amina! Ni tamshi la namna gani! "Hayo ndiyo, Maandiko, yanayowashuhudia kwamba Mimi ni Nani," akasema Yesu.

59 Na Maandiko ndiyo yanayowaambia saa tunayoishi. Na mambo mnayoona yanafanywa, ni Mungu Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Hakuna kinachoweza kuwafufua wafu ila Mungu. Hakuna kinachoweza kufanya mambo ambayo Yeye anafanya sasa ila Yeye. Kwa kuwa Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

60 Sasa tunaona ule mwelekeo wa sasa wa watu, basi, "Loo! siku zimepita, hakuna kitu kama miujiza. Hao watu wote wanasisimkwa kimwili."

61 Hebu msikilizeni huyo Eliya, nabii, akiwakemea pamoja na wanatheolojia wao. Angalieni, angalieni, alinena kana kwamba Yeye alikuwa ndiye Mungu Mwenyewe. Eliya alinena kana kwamba yeye alikuwa ndiye Mungu Mwenyewe, "Umande hautaanguka kutoka mbinguni mpaka nitakapouagiza." Amina! Ndiyo, bwana. Huyo nabii alikuwa amekaa kwa muda mrefu sana katika Uwepo wa Mungu!

62 Manabii wa Agano la Kale, ama wa wakati wo wote, walipoishi katika Uwepo wa Mungu mpaka wakawa Neno, Ujumbe wao ni Neno Lenyewe. Pia, kumbukeni, yeye alisema, "BWANA ASEMA HIVI." Na wakati watu hao walipokuwa na jumbe hizo kutoka kwa Mungu, nao wakaingia kwenye kilindi sana hata mawazo yao wenyewe . . . Huenda ilikuwa ni kinyume cha mawazo yao, huenda wao wasingeweza ku— kuliona kuwa ni sawa. Lakini walikuwa wakinena Neno la Mungu, "BWANA ASEMA HIVI."

63 "Hakutakuweko na mvua yo yote mpaka nitakapoiagiza." Loo, ni tamshi la namna gani! Yeye alikuwa katika Uwepo wa Mungu naye alikuwa amekwisha kuthibitishwa kinaganaga kabisa. Pia, kumbukeni, jambo hilo pia linafuata Amosi 3:7, "Bwana Mungu hatafanya neno lo lote mpaka kwanza awafunulie watumishi Wake manabii." Kasema, "Hakutanyesha mvua yo yote!" Yeye kwanza . . .

64 Wakamcheka, walimdhania ni mwenda wazimu, "Huyo mwenda wazimu!" Lakini, mnaona, yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI ya kwamba haitanyesha. Na, Mungu, kabla hajafanya jambo hilo, Yeye alimfunulia Eliya mtumishi Wake.

Naye alikuwa nabii aliyethibitishwa, aliyehakikishwa, kwa hiyo watu walipaswa kutubu. Lakini, badala ya jambo hilo, walimcheka, wakasema, "Loo, tuna mvua tele! Mabirika yamejaa. Mito inatiririka vizuri."

65 Biblia ilisema ya kwamba, "Hakukuwa hata na umande kwa miaka mitatu na miezi sita." Vijito vyote na maji vilikauka, kila mahali. Hiyo haikuwa mtu huyo, hiyo ilikuwa ni Mungu akizungumza kupitia mtu huyo. Huyo alikuwa ni yule "MIMI" aliyekuweko. Daima tunajua. Kwa hiyo yeye . . .

66 Tunaona ya kwamba mtu anapokuja, ametumwa kutoka kwa Mungu, amechaguliwa na Mungu, akiwa na BWANA ASEMA HIVI ya kweli, ujumbe huo na mjumbe huyo ni mmoja na kitu kimoja. Kwa sababu yeye ametumwa kuwakilisha BWANA ASEMA HIVI, Neno kwa Neno, kwa hiyo yeye pamoja na ujumbe wake ni mmoja.

67 Mtu wa kimadhehebu chini ya uongozi wa kimadhehebu, yeye na kanisa hilo ni "mmoja." Mwanatheolojia chini ya theolojia, iliyobuniwa na madhehebu fulani, yeye na ujumbe wake ni mmoja; kanisa la theolojia, mwanatheolojia. Ni kweli.

68 Basi wakati mtu anapokuja na BWANA ASEMA HIVI, yeye na Ujumbe huo ni mmoja. Na wakati Eliya alipokuja na BWANA ASEMA HIVI, yeye na ujumbe wake wakawa kitu kimoja. Kama tu vile Yesu, wakati alipokuja, Yeye alikuwa ni Neno, Yohana Mtakatifu 1. Kwa hiyo Neno la Mungu na mjumbe wa wakati ule walikuwa ni kitu kile kile, daima. Hiyo ni kweli.

69 Yesu alikuwa ni Neno lililotabiriwa. Yeye alikuwa kile manabii walichosema kingetukia, "Bikira atachukua mimba na atamzaa Mtoto huyu." Nyuma huko hapo mwanzo, Mungu aliwaambia, kasema, "Uzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka, naye atamponda kisigino." Nabii hizi zote zilikuwa zimetolewa. Daudi akilia, manabii wote waliosalia katika nyakati zote, wakinena juu Yake. Yeye alikuwa Ndiye hilo Neno lililodhihirishwa! Haleluya!

70 Sasa mnaona mahali ninapojaribu kufikia? Nilizungumza nanyi waziwazi sana asubuhi ya leo. Hivi hamwoni mamlaka ya Mungu aliye hai katika Kanisa lililo hai, Bibi-arusi? Wagonjwa wanaponywa, wafu wanafufuliwa, viwete wanatembea, vipofu wanaona, Injili inatangazwa katika nguvu Zake, kwa maana Ujumbe na mjumbe ni kitu kimoja. Neno liko ndani ya Kanisa, katika mtu.

71 Neno la Mungu lilikuwa ndani ya Eliya wakati alipotembea kule akiwa na BWANA ASEMA HIVI, na kusema, "Haitanyesha." Huyo hakuwa Eliya; huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Eliya.

72 Nilisema mara nyingi, kama vile yule mama wa Christian Science alivyoniambia wakati mmoja. Nimesimulia kisa hicho

mara nyingi. Yeye alisema, "Bw. Branham, unajisifia sana juu ya Yesu."

Nikasema, "Ninatumaini hilo ndilo jambo tu nitakalowajibika kwalo."

Naye akasema, "Wewe unajaribu kumfanya ni Mungu."

Nikasema, "Yeye alikuwa Mungu."

73 Kasema, "Loo, Yeye alikuwa ni nabii, alikuwa ni mtu mzuri, bali Yeye hakuwa Mungu."

74 Nami nikasema, "Vema, nionyeshe Andiko moja ambalo linasema Yeye hakuwa."

75 Akasema, "Katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, inasema ya kwamba Yeye "alilia" alipoenda kwenye kaburi la Lazaro."

76 "Vema," nikasema, "hakika, Yeye alilia. Yeye alikuwa wote wawili mwanadamu na Mungu. Yeye alikuwa mwanadamu, akilia; bali ilimbidi awe Mungu ili awafufue wafu." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Yeye alikuwa mwanadamu, alipokuwa ana njaa; bali alikuwa Mungu alipowalisha watu elfu tano, akiwa na biskuti chache na samaki watano." Hiyo ni kweli. "Yeye alikuwa mwanadamu, alipolala nyuma ya ule mtumbwi; bali ilikuwa ni Mungu ndani Yake ambaye angeweza kutuliza maji." Kwa nini? Yeye na Ujumbe Wake walikuwa mmoja.

77 Yeye alisema, "Mimi na Baba Yangu ni mmoja. Baba Yangu anakaa ndani Yangu." Alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.

78 Nafikiri lilikuwa ni jambo la kushangaza sana juzi juzi, wakati nilipokuwa nikileta *Nyakati Saba Za Kanisa*. Kwanza, si—sikuweza kuelewa Yesu amesimama pale akiwa na hizo... akiwa na hizo nyeupe juu Yake namna hiyo, nikasema, "Nywele Zake zilikuwa nyeupe kama theluji." Sikuweza kuelewa jinsi mtu mwenye umri wa miaka thelathini na mitatu angekuwa na nywele nyeupe theluji.

79 Nikampigia simu mwanatheolojia stadi, mwanatheolojia Mpentekoste, rafiki wangu msiri. Vema, ilikuwa ni Ndugu Jack Moore. Yeye ni mtu mwerevu, mwenye akili. Akasema, "Ndugu Branham, huyo alikuwa ni Yesu aliyetukuzwa. Hivyo ndivyo alivyoonekana baada ya kutukuzwa." La, sikuweza kuamini jambo hilo. La.

Ni—ni—nikasema, "Vema, Ndugu Moore, asante."

80 Niliingia chumbani kule nikaanza kuzungumza na Mungu. Nikachunguza kamusi yangu kumrudisha nyuma hadi kwa Danieli, ambapo ilisema, "Naye akaja kwa Mzee wa Siku Ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu." Nikasema, "Bwana, si—si—sijui la kusema, nami nina wajibu." Sasa, hiyo ilikuwa kabla ya zile mu-...na kumbukeni, kabla ya zile

Muhuri Saba kufunguliwa, mwaka mmoja ama zaidi, hapo kabla. Nilikuwa ninaomba kule, "Bwana, ilikuwa ni nini?"

81 Nami nikaangalia, akisimama mbele zangu, na pale alisimama mtu na alikuwa hakimu, naye alikuwa amevaa wigi nyeupe. Wale mahakimu wa zamani za kale walikuwa wanavaa wigi nyeupe kuonyesha ya kwamba yeye alikuwa mamlaka kuu.

82 Na basi nilipomwona Yesu amevaa wigi nyeupe, nilisema inathibitisha tu ukweli ambao tunajua, ya kwamba Yeye ndiye Mamlaka Kuu. Mungu alishuhudia jambo lile lile kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura, kasema, "Huyu ni Mwanangu ninayempenda, msikieni Yeye, Mamlaka Kuu!"

83 Halafu nyuma kule kwenye mwanzo wa zile Muhuri Saba, wakati hao Malaika saba waliposhuka katika umbo la hilo piramidi, wakasimama pale na kuniambia nirudi hapa na kuzungumza juu ya hizo Muhuri Saba, Naye angekuwa pamoja nami. Yeye alinionyesha zilikuwa ni nini, yale mambo yaliyopotea. Sikuzote mimi nilifikiria kimetiwa muhuri nyuma ya Kitabu na lingekuwa ni jambo ambalo halikuandikwa kwenye Kitabu, lakini ikawa kwamba ilijulikana ya kwamba Yeye hawezi kufanya jambo hilo. Si jambo ambalo limeandikwa ndani ya Kitabu . . . Ni jambo lililofichwa ndani ya Kitabu hicho. "Kwa kuwa mtu atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake au kuongeza neno moja Kwake . . . " Kwa hiyo ni siri ambayo ilikuwa ndani ya Kitabu kile katika hizi nyakati saba za kanisa. Kila moja ya hizo ilitoa si—siri, yote kuhusu ubatizo wa maji na mambo haya mengine ambayo wao wamepapasa-papasa kwa muda mrefu sana.

84 Basi wakati hilo lilipopanda juu, vile vyumba vikubwa vya uchunguzi kutoka huko California, mpaka huko Mexico, kule Tucson, kila mahali, walipiga picha Yake. Lilikuwa ni tamasha la ajabu. Ndugu Fred Sothmann pale, anayeketi nyuma kule kabisa, na mimi pamoja na Ndugu Gene Norman, waliokuwa wamesimama papo hapo wakati lilipopanda juu. Wao walipiga picha, bado hawajui ni kitu gani. Hapa muda fulani uliopita, kila mtu akisema, "Angalia hapa. Hii inaonekana namna *hii*, na hayo mabawa ya Malaika, jinsi yalivyojikunja humo ndani."

85 Siku moja, nilipoigeuza upande wa kulia, nilipoiangalia, huyo hapo Yesu Kristo kikamilifu kabisa kama vile Hofmann alivyowahi kumchora. Alikuwa amesimama pale akiwa amevaa wigi nyeupe, akiangalia nyuma chini duniani, ikionyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mamlaka Kuu. Mbingu zinatangaza jambo hilo, Biblia inalitangaza, Ujumbe unalitangaza. Yote ni jambo lile lile. Mamlaka Kuu, akiwa amevaa wigi nyeupe; unaona ndevu zake nyeusi chini yake. Wengi wenu mmeiona picha hiyo. Tunayo kule nyuma. Hebu igeuzie tu kulia, upande, iangalie. Huyo hapo, kikamilifu tu kama vile ingalikuwa, kama vile angalikuwa kwamba amepigwa picha. Wao wanaiangalia

kutoka upande mbaya. Unapaswa kuiangalia kutoka upande ulio sahihi. Na ni Bwana Mungu tu anayeweza kufunua ni upande gani ulio sahihi. Igeuzie kulia kwako uiangalie. Huyo hapo, kikamilifu kabisa, kana kwamba alipigiwa picha kule juu.

86 Mara ya kwanza niliyopata kumwona, Yeye alionekana kama *Kichwa cha*. . .Hofmann. Mimi sikuwa nimeiona hiyo hapo kabla. Na kwenye maskani ya Billy Sunday, miaka kadha baadaye, niliiona. Nyumba yangu haijapata kuwa bila ya moja ya picha hizo tangu wakati huo.

87 Halafu, huku angani, nikisema ya kwamba Mungu yeye yule niliyemwona juu katika ono hapa nje, nikiwa tu kijana mwanamume mdogo hapo nje karibu na pale jengo hili la shule linaposimama, Yeye alionekana namna hiyo. Na hapa Mbinguni, miaka thelathini na mitatu baadaye, inalitangaza, ya kwamba ni kweli. Hivyo ndivyo anavyoonekana; si kitu fulani cha kisiri cha wazo la mtu fulani.

88 Kama vile kule Vatican, wao wana Kri—Kri—Kristo aliyechorwa kule, akiwa na mzingo mdogo mweupe wa ndevu ama mzingo wa ndevu kukizunguka kidevu Chake, urefu wa kama nusu inchi, kinazunguka upande wa juu wa mdomo Wake na namna *hii*, wanamwita huyo Kristo.

89 Hilo linanikumbusha tu juu ya msanii Myunani niliyemwona wakati mmoja katika kanisa moja la kale la jimbo, akionyesha jinsi Adamu na Hawa walivyoonekana; walionekana kama hayawani ama cho chote kile. Hivyo ndivyo akili ya kimwili inavyoweza kufahamu jambo fulani la kiroho. Nafikiri Adamu alikuwa mwanamume aliyekuwa mzuri kuliko wote waliopata kuishi, naye Hawa alikuwa mwanamke mkamilifu kabisa katika kila hali.

90 Sasa watu wa kimwili wanalifungafunga jambo Hilo katika mawazo yao wenyewe, kisha Mungu hutuma chini na kulifunua jambo Hilo kwa Uweza Wake. Hilo ndilo hasa lililotukia hapa katika siku za Ahabu.

91 Sasa, tunaona kwamba Eliya aliweza kusema jambo hilo kwa sababu Ujumbe wa saa hiyo na Neno la Mungu. . . Yule mjumbe, ule Ujumbe—Ujumbe, na Neno, walikuwa mmoja kabisa. Nabii, Neno, Ujumbe; mjumbe, Ujumbe, na Ujumbe, walikuwa mmoja. Yesu alisema, "Kama sizitendi kazi nilizoandikiwa, basi msiniamini." Hilo ni zuri. Mtu ye yote na ujumbe wake ni mmoja.

92 Hiyo ndiyo sababu ya kwamba leo wao hawaamini katika kuzitenda kazi za Mungu, kwa sababu wao hawaukubali Ujumbe wa Mungu. Wao hawaumini Ujumbe.

93 Lakini wale wanaoamini saa ya Mungu tunayoishi, mambo haya ni Chakula kilichofichwa. Hebu wazieni tu, Munguameficha Hilo kiasi kwamba ingawa wao wanaliangalia moja kwa moja hata hivyo hawalioni. Jinsi ile ile Eliya alivyolipofusha

jeshi la Shamu. Jinsi ile ile Mungu anavyompofusha asiyeamini asione Chakula halisi cha mtoto, mwamini.

94 Ijapo walimwita Nuhu, "mshupavu wa dini," akijenga safina, macho yake yalikuwa yamefunguliwa kwa Neno la Mungu na ahadi. Kitu kile kile walichoita ushupavu wa dini, kilimwokoa Nuhu na jamaa yake. Mnaona, kitu kile kile. Kitu kile watu wanachokicheka, ndicho kitu tunachokiomba. Kile kitu ambacho watu wanaita "wenda wazimu," tunakiita "Kikuu!" Kile ulimwengu unachoita "kikuu," Mungu anakiita "Upuuzi!" Na kile ulimwengu unachoita "kijinga," Mungu anakiita "Kikuu!" Ni kinyume hasa cha Kweli na uongo. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

95 Kumbukeni, yeye aliendा akaingia mahali pake pa siri kwa mpango wa Mungu, kwa wito wa Mungu, na kwa Neno la Mungu. Eliya aliingia katika mahali pake pa siri kwa kutangulia kujua kwa Mungu (mpango), na wito katika maisha yake, na kulingana na Neno. Kama hivyo sivyo jinsi tulivyoingia, sijui kwa nini tunafika kule.

96 Basi angalia, kabla ukame haujaanza, Eliya aliingia katika mahali hapa pa siri apate kuishi. Mfano halisi wa kabla ya hukumu kuanza kuipiga nchi, Kanisa tayari limekwisha itwa litoke, Bibi-arusi tayari amechaguliwa, na anangojea tu kabla hukumu haijapiga. Tayari anangojea, akila Chakula cha Mungu, akifurahia baraka za Mungu. Mtu ye yote katika akili yake timamu anajua ya kwamba tunaelekea moja kwa moja, tuko hasa kwenye ile saa ya hukumu kabisa.

97 Angalia! Ndugu Banks, wengi wenu ninyi watu mlio hapa usiku wa leo, na mliokuwa mmesimama kule nje kwenye ule mlima asubuhi ile.

98 Basi ninataka kuzungumza kuhusu ule mlima, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda. Nina ufunuo mkubwa, kitu kingine zaidi ambacho ni vigumu kujizuia kuwaambieni usiku wa leo. Lakini nina . . . Mnaona? Na daima inaendelea, wakati wote, jambo moja likitukia baada ya lingine. Mnaona? Halitakosa kutukia, kwa maana ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI.

99 Kila mmoja wenu hapa, maelfu mara elfu kwenye kanda, wamenisikia nikisimama na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, itakuwa hivi na hivi." Na hata magezeti na magazeti ya juma hayana budi kutangaza jambo hilo ya kuwa ni kweli. Wao hawajui ni kitu gani, bali wameliona. Wao hawajui ni kitu gani, bali wameona jambo hilo likionyesha Neno kuwa ni la Kweli kabisa.

100 Tulikuwa tumesimama hapa chini mtoni, yule Malaika wa Bwana akashuka siku hiyo, miaka thelathini na mitatu, ama ilikuwa ni mwaka wa 1933, akashuka na akanena mambo yale aliyonena. Nikatoka, na watu wengi wamesimama ukingoni pale, wakasema, "Jambo hilo lilikuwa na maana gani, Billy?"

101 Nikasema, “Hilo halikuwa kwa ajili yangu mimi; hilo lilikuwa ni kwa ajili yenu. Mimi ninaamini; ninyi hamwamini.” Na nikaendelea kwenda tu.

102 Ndipo mchungaji akaniambia, akasema, “Una maana ya kwamba wewe, ukiwa na elimu ya darasa la saba, utazunguka ulimwenguni kote na kuwaombea wafalme na watawala na wafalme na kadhalika? Na, loo!” kasema, “sahau jambo Hilo!”

103 Nisingeweza kulisahau Hilo, lilikuwa limechorwa moyoni mwangu. Sasa hapa, miaka thelathini na mitatu baadaye, kila alilosema limetukia kikamilifu jinsi alivyosema Yeye angefanya. Yeye ni Mungu naye hawezi kushindwa. Yeye daima hutimiza Neno Lake. Yeye . . . Usije kamwe ukalititilia shaka.

104 Sasa, angalia, yeye aliingia kule kwa mpango wa Mungu (kujua tangu zamani), wito wa Mungu, na Neno la Mungu, naye akaingia kabla ya ukame kuanza.

Sasa, tunajua ya kwamba hukumu iko tayari kupiga.

105 Wakati nimesimama juu ya kile kilima siku ile, Ndugu Banks Woods akiwa amesimama hapa, tulikuwa tunakwea kile kilima. Labda nilinukuu tena, ili kwamba niijenge imani yenu kwa ajili ya mstari huu wa maombi ambao uko karibu kuanza katika dakika zingine kumi, kumi na tano zinazofuata. Nilikuwa tu ninatembea mbele ya Ndugu Banks. Yeye alikuwa . . . Nafikiri alikuwa amemwacha Dada Ruby ambapo alikuwa mgonjwa. Naye alikuwa ananifuata, nikaona uso wake, mwekundu. Nikaangalia nyuma. Nikafikiri labda kilima kitakuwa kigumu kwake kupanda, kwa hiyo kwa namna fulani nikapunguza mwendo. Huko huko jangwani, huko juu ya vilima namna *hiyo*, pahali pale pale ambapo wale Malaika wa Bwana walitokea. Tulikuwa tunaelekea moja kwa moja upande huo wakati huo, mahali walipotokea miezi michache kabla ya jambo hilo.

106 Na wakati nilipokuwa ninapanda kile kilima, Roho wa Mungu . . . Nilipogeuka, nikaangalia juu ya mlima, Yeye alisema, “Okota jiwe lile, na umwambie, ‘BWANA ASEMA HIVI, utauona Utukufu wa Mungu katika masaa machache yafuatayo.’”

107 Nikaokota tu lile jiwe, na kusema, “Ndugu Banks, sijui ni kwa nini,” nikalitupa hewani, na nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, utaona Utukufu wa Mungu.”

Akasema, “Hilo linamaanisha Ruby?”

108 Nikasema, “La, sidhani lilikuwa na uhusiano wo wote nawe, Banks au Ruby, ye yote wenu. Ninafikiria tu Yeye alikuwa tu anasema “BWANA ASEMA HIVI, jambo fulani litatukia.”

109 Na asubuhi yake tulipokuwa tumesimama pale, wengi wa hao wanaume, sijui ni wangapi wanaoketi hapa sasa, tulikuwa watu kumi na wawili ama kumi na wanne, kumi na watano tulioketi pale. Mara, mhudumu akanijia na kusema,” “Ndugu

Branham," akasema, "jina langu ni *fulani*." Kasema, "Mimi nilikuwa mmoja wa wadhamini wako California."

110 Nikasema, "Nina furaha kukutana nawe, bwana." Douglas McHughes. Akasema, "Mimi . . . " Nikasema, "Nina furaha kukutana nawe." Tukapeana mikono.

111 Akasema, "Vema, sasa, nataka kukuuliza swali." Kasema . . . Roy Roberson, mdhamini hapa; Ndugu Woods, Terry na Billy, na, loo! Ndugu Mc Anally, na sijui ni akina nani wote waliokuwa wamesimama pale. Ndipo nikaninii . . . Yeye akasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani." Akasema, "Hivi Bwana hukupa maono huku nje namna hii?"

112 Nikasema, "Ndiyo, ndugu, lakini mimi huja huku nje ili kwa namna fulani nipate kuliepa jambo hilo, ili nipumzike."

Ndipo nikageuka namna *hii* kuangalia, na nikaona daktari mnene akimwangalia, akasema, "Kasisi McHughes, ugonjwa huu kwenye jicho lako hivi karibuni utaliharibu jicho lako. Nimekutibu kwa miaka miwili, na siwezi kufanya kitu cho chote juu yake."

Ndipo nikageuka nikamwangalia. Nikasema, "Sababu ya wewe kuniuliza jambo hilo, daktari wako alikwambia, juzijuzi, Ugonjwa huo ulikuwa kwenye jicho lako.'" Ilikuwa mchana, kama saa tano, naye alikuwa amevaa miwani ya jua. Ndipo nikasema, "Sababu yake; wewe huvai hiyo kwa sababu ya jua, ni kwa sababu ya jicho lako. Yeye alikwambia ya kwamba 'utapoteza hilo jicho.'"

Naye akaanza kulia, kasema, "Hiyo ni kweli."

113 Nikageuka na kutembea-tembea hapo karibu tena, nilikuwa na sepetu mkononi mwangu. (Nami kikaangalia; nikamwona yeye amesimama pale akiniangalia, macho yake maangavu kabisa.) Nikasema, "Lakini BWANA ASEMA HIVI, hutapoteza hilo jicho." Nilikuwa nikiwinda pamoja naye mwishoni mwa mwaka huu, yeye anaweza kuona vizuri zaidi kuliko mimi na kila mtu kwenye lile kundi. Yeye kamwe. . . .

114 Kisha nikaona bibi mzee akitelemsha soksi yake na kuinua upindo wa rinda lake. Akasema, "Mwanangu, ukimwona Ndugu Branham, mwambie aombee miguu yangu." Ndipo nikaangalia pale chini, na kidogo . . . ilionekana kama ni vivimbe vikining'inia kila mahali miguuni mwake.

115 Nikasema, "Mama yako ni bibi mwenye nywele zenye mvi. 'Mwanangu,' unaona. Alikwambia kabla ya kuondoka, kama ukiniona, uniambie nimwombee miguu yake. Ana vivimbe vidogo-vidogo, vitu kama hivyo, vinavyoning'inia kila mahali kwenye miguu yake." Karibu azimie.

Kasema, "Hiyo ni kweli."

Nikasema, "Mwambie asiwe na wasiwasi. Itakwisha."

116 Nikaanza kuzungukazunguka. Ndipo nikasikia Sauti ya Mungu ikinena, kasema, "Ondokeni, upesi."

Roy Roberson akiwa amesimama pale, nikijua alikuwa shujaa wa vita, nikaweka mkono wangu juu ya bega lake, nikasema, "Ndugu Roy, jificheni, haraka mwezavyo!"

Kasema, "Kuna nini?"

Nikasema, "Ondokeni! Jificheni!"

117 Nami nikaanza tu kutembea-tembea, nikaweka chini sepetu langu, nikageuka, nikavua kofia yangu. Na mara Huyu hapa anakuja, Utukufu wa Mungu ukishuka katika upepo wa kisulisuli ulioipasua sehemu moja ya mlima namna hiyo, na ukalipua na kupatikisa mahali pale namna hiyo, ukakata vilele vya vichaka; kama tu futi tatu ama nne, futi tano juu ya kichwa changu. Ukarudi kama upepo wa kisulisuli namna hiyo; ukalipua tena. Na, huu hapa unakuja, mara tatu.

118 Ndipo wakati ulipoondoka, mara ya tatu, Ndugu Banks akaja, akasema, "Hilo ndilo ulilokuwa unazungumzia?"

Nikasema, "Ndiyo."

Kasema, "Ilikuwa ni nini?"

119 Nikasema, "Mungu hutokea katika pepo za kisulisuli." Sikujua kama Yeye alitaka niwaambie watu ama nisiwaambie.

120 Halafu nikaenda na kuomba kidogo. Ndipo akaniambia ningeweza kuwaambia. Nikasema, "Ni hukumu itakayopiga Pwani ya Magharibi." Iangalie leo! Angalia yaliyotukia masaa machache baada ya jambo hilo: Alaska ilizama. Na sasa yote nzima inazama. Tunaingia hukumuni. Rehema imekataliwa.

121 Lakini Mungu ashukuriwe, tuna Chakula kilichofichwa, Chakula cha kiroho, hata tunaishi kwa fadhili na rehema za ufunuo wa Yesu Kristo katika siku hizi za mwisho, akijithibitisha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Amina! Wao waliingia. Eliya aliingia kabla ukame kuanza. Mungu ashukuriwe kwa kuwemo ndani kabla hukumu kuanza. Sasa ni wakati wa kutoka na kuingia, kutoka kwenye hayo madhehebu na kuingia katika Kristo, wakati wa kutoka na kuingia kwa waamini wote wa kweli.

122 Kisha akaitwa, na akakaa humo ndani. Kumbuka, yeye hakuondoka kwenye kile kijito mpaka Mungu alipomwita.

123 Na baada ya ukame kuwa unakaribia kwisha, Yeye alimwita kutoka kule, aende kwenye nyumba ya mjane. Angalia, Yeye alimwita huyu mjane. Na mjane huyu hakuwa ameshirikiana na wasioamini; akachukua alama ya mnyama katika wakati wa ukame. Kwa hiyo Yeye alimwita atoke kuninii . . . akamwita Eliya apate kumlisha huyu mjane. Walikuwa tu na keki moja ndogo, kitu kimoja kidogo yule mama alichokuwa anashikilia. Ndipo Eliya akasema, "Nipe hicho mimi, kwanza. Kwa kuwa,

BWANA ASEMA HIVI, lile pipa halitapunguka wala ile chupa haitaisha, hata siku ile Bwana Mungu atakapoleta mvua juu ya nchi." Kumweka Mungu kwanza, Neno Lake kwanza!

124 Angalia, kulikuweko na unga kwenye pipa. Kila alipoenda kuchota unga, kulikuweko na unga kwenye pipa. Kulikuweko na mafuta kwenye chupa, kila wakati alipoenda kumimina. Kwa nini? Unga ulimwakilisha Kristo katika ile sadaka ya unga. Mbegu zilipaswa kuwekwa sawa kabisa, kusaga kila moja. Kila mbegu ya huu unga hulingana na nyingine kabisa, ikionyesha ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hilo lilikuwa ni Neno, Chakula cha Uzima kikiufuata ujumbe huo, kuthibitisha Neno.

125 Ndivyo ilivyo leo, enyi marafiki. Ndivyo ilivyo leo, ya kwamba Chakula cha Uzima ambacho watoto wanakula, kinafuata Ujumbe wa Mungu, kuwahifadhi katika wakati wa ukame. Vipi kama Yeye angalisimama mbele zetu leo? Vipi kama Yeye angalisimama mbele hivi sasa? Yeye angetenda na kufanya vile vile hasa kama alivyofanya wakati Yeye alipokuwa katika mwili hapa duniani. Bibi-arusi ni sehemu ya Mume, Kanisa ni sawa na Kristo. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Na Neno ndilo lililofanya jambo hilo. Yeye alitwambia ya kwamba mambo ambayo Yeye alifanya sisi nasi tungeyafanya.

126 Tunaona hapa tena, kama Neno limo ndani yetu na limetujia, kama lilivyofanya kwa Eliya katika siku ile, litafanya jambo lile lile alilofanya, yeye angekula Mambo ya siri ya Mungu ambayo ulimwengu umefichwa. Loo! Tena, jambo hilo linaufanya Ujumbe na mjumbe kuwa ni kitu kimoja. Chakula cha kiroho kiko tayari, na kiko katika wakati wake sasa. Na kila mmoja wenu anaweza kupata Chakula hiki kama ukikitaka, kama uko tayari kuondoka kwenye kutokuamini kote kwa wakati huu, kama uko tayari kuingia katika Kristo, kuingia katika ahadi Yake.

Pia kumbuka ahadi Zake, katika Malaki 4, Luka 17:30, pia katika Yohana Mtakatifu 14:12, na sijui ni Maandiko mengine mangapi, ya kutaja, Yoeli 2:38, na yote ambayo Yeye angefanya, ama 2:28, hasa, yale Yeye angefanya katika siku hizi za mwisho. Na jinsi nabii alivyosema ya kwamba kungekuwako Nuru katika siku hizi za mwisho, jinsi jambo hilo lingetenda kazi, kile lingefanya, Maandiko yote yakielekeza kwenye siku hizi za mwisho. Na huyo ni Kristo! Kama unaweza kujificha Humo sasa, katika Mahali hapo pa siri, unaweza kula na kuona fadhili na rehema za Mungu. Kama wewe ni mgonjwa, kuna kuponya pale.

127 Mnakumbuka wakati Elisha, baadaye, alikuwa ameagiza . . . Baada ya ile sadaka ya unga ambayo alitoa, Kristo, na kuihifadhi nyumba ya mjane kwa Hiyo. Angalia baadaye kidogo wakati alipoagiza moto kutoka mbinguni, na kadhalika, na kuthibitisha kutumwa kwake, na Mungu, Roho ya nabii.

128 Angalia kule jangwani, alipokuwa amelala kule chini ya mreteni, Malaika alishuka akiwa na unga ule ule, akaoka keki na kumlisha. Na baadaye kidogo akamlaza usingizi tena, kisha akamwamsha, na alikuwa ameoka keki nyingine za unga pale kwa ajili yake. Naye akaenda kwa nguvu za keki hizo siku arobaini. Mungu atukuzwe! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, jinsi tunavyompenda Yeye, Chakula cha rohoni katika wakati Wake!

129 "Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwapa mbwa." Je! Yesu hakuwaambia wanawake Wasirofoinike jambo lile lile? Yeye alitumwa kwa Walio Wake. Hiyo ni kweli. Na hao ndio aliowajia . . . Yeye kamwe hakuwaendea Mataifa.

130 Na sasa leo Yeye anawazuru Mataifa katika wakati wao, na si vema . . .

131 Mnasema, "Hivi kwa nini Ujumbe huu hauendi huko nje kwenye sehemu hizi maarufu kubwa kubwa, mikutano hii mikubwa, kama vile miongoni mwa madhehebu?"

132 Si Chakula chao. Si Chakula cha linalojiita kanisa. Ni Chakula cha Bibi-arusi. Ni Chakula cha rohoni kwa wakati wake. Kingewachefua tumbo. Ni kinono mno kwao. Mnaona? Mnaona? Hu—hu—huwezi kufanya jambo hilo. Lakini, kwa watoto, Hicho ni Mkate, Hicho ni Uzima, Hicho ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

133 Tutachelewa sana kama hatuanzi mstari wa maombi sasa, kwa hiyo hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

134 Mungu mpenzi, Chakula kwa wakati wake, Chakula cha kiroho. Kitu fulani ambacho ulimwengu haujui kitu juu yake. Jinsi tunavyomsikia Bwana wetu akisema usiku ule, ama siku ile kule Samaria, mahali pale pale ambapo Elisha alitembea na kusema, "Mbona, umande hautaanguka mpaka nitakapouagiza." Huyu hapa amesimama pale Yesu akiwaambia wanafunzi Wake.

Kasema, "Bwana, mbona Wewe huli?"

Akasema, "Mimi ninacho Chakula msichokijua ninyi."

135 Kweli, Bwana, Chakula Chake kilikuwa ni kuyatenda mapenzi ya Mungu, kuona kazi za Mungu zikidhihirishwa katika wakati Wake. Yeye alikuwa pale kuhakikisha ya kwamba zimetendeka. "Sitendi neno asiponionyesha Baba Yangu kwanza. Yale anionyeshayo Baba Yangu, hayo nayafanya."

136 Na, Baba, ndivyo ilivyo leo. Kanisa, mwamini wa kweli, Mwili wa waamini, wana ruhusa ya kukikaribia Chakula, Chakula cha rohoni, ambacho hao wa kawaida hawakijui kamwe. Ulimwengu haujui kitu juu ya Chakula hiki, Baba. Lakini Kanisa Lako, watu Wako, Bibi-arusi wa Mwanao, anakipenda.

137 Tuna njia ya kufikia kuponywa kwa miili yetu wakati madaktari wameshindwa. Tuna njia kwa jambo hili. Ni kimoja cha Vyakula vya Mungu, ambavyo alililipa Kanisa Lake, na kukiahidia watoto Wake waaminio katika siku ya mwisho. Basi, Baba, tusaidie tuwe watoto waaminio, kwa maana mambo yote yanawezekana kwa waamini. Tujalie, Mungu mpenzi. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

138 Ninaamini Billy aliniambia ya kwamba wametoa kadi za maombi. Kama mtu fulani angeniambia herufi iliyo kwenye kadi ya maombi, hiyo tu ndiyo ninayohitaji. [Mtu fulani anasema, "C."—Mh.] C, vema, hebu tuchukue C, moja, tuanze, mpaka nitakapoanzisha mstari wetu. Mnaona, sasa, huenda wao wakawa kila mahali. Sasa, kama kila mtu . . . Vema, mnaona, nitajaribu jambo hili. Sijui kama tunaweza kulifanya ama hatuwezi. Au tunaweza kuwa tu na mstari wa kuita; mketi kimya. Ni mamoja kwangu. Kama ingefaa kuja hapa jukwaani, ama mfanye mstari wa kuitwa, ni mamoja kwangu, njia yo yote ile. Mimi ninamtegemea tu Roho Mtakatifu peke Yake. Ninamtegemea Yeye kulitetea hili Neno ambalo nimehubiri.

139 Ndugu George Wright, ninaamini jambo Hilo. Tangu nilipokuwa mtoto mdogo, nikija nyumbani kwako miaka mingi iliyopita, nikisikiliza maskini yule ndege akiimba mtini, ningali ninaamini Ujumbe ule ule. Ninaamini ni ule ule.

140 Vema, ninaona kule nyuma wanatoa nafasi kwa ajili ya mstari wa maombi. Vema, kadi ya maombi C, namba moja, mbili, tatu, nne, tano, njoni kwanza na msimame papa hapa. Endapo huwezi kusimama, kama utainua tu mikono yako, wengine wao watakuja kukubeba. [Mtu fulani anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Ati nini? Naam. A-ha. Kadi ya maombi C, moja, mbili, tatu, nne, tano. Na sasa angalieni, ninyi msio na kadi ya maombi . . .

141 Sasa, sijawahi kuwa na mstari wa maombi wa namna hii kwa muda mrefu, mrefu sana. Ni wangapi wanakumbuka agizo langu wakati tulipoyajenga Maskani hapa? Kasema, "Fanya kazi ya mhubiri wa injili." Hakusema nilikuwa mhubiri wa injili. Alisema, "Fanya kazi ya mhubiri wa injili," mnaona, "kwa maana wakati unakuja ambapo jambo hilo litabadilishwa." Saa hiyo yaja. Vema. Sasa, katika jambo hili, Yeye . . .

142 Huwezi kuchanganya huduma mbili ama huduma tatu mbalimbali pamoja, kuwa mchungaji na kuhubiri injili, wakati ule ule. Huwezi kuwa na—nabii na labda mchungaji, wakati ule ule, unaona, maana una kazi mbalimbali, huduma mbalimbali.

143 Lakini Bwana alinipa jambo ninalopaswa kufanya katika Ujumbe wangu. Lakini basi Yeye alisema, "Fanya kazi ya mhubiri wa injili, timiliza huduma yako, kwa maana utakuja wakati watakpoyakataa Mafundisho yenye uzima." Kama jambo hilo halijatukia sasa! Kila kanisa la kimadhehebu limenikataa. Wao hawangevumilia Mafundisho yenye uzima.

"Ila kwa kuzifuata tamaa zao wenyewe watajipatia waalimu, nao watazigeukia hadithi za uongo. Nao watafanya mambo makubwa na makuu kama Yambre na Yane waliompinga Musa, lakini upumbavu wao utajulikana kwa watu wote." Mnaona? Mnaona? Vema, kuigiza! Mnaona jinsi Yambre . . .

144 Na, Mungu Mbinguni anajua, jambo hilo liko pale pale pembeni mwa lile jiwe la Maskani tangu mwaka wa 1933, limeandikwa kwenye ukurasa wa Biblia, liko pale pale. Angalia jinsi walivyolitenda jambo hilo. Angalia yaliyotukia. Uigaji, vile vile kabisa. Kasema, "Waache, upumbavu wao utajulikana kama vile wa Yane na Yambre ulivyojulikana." Tumefikia siku hiyo.

145 Nililiona kanisa wakati huo tulipokuwa tukiweka jiwe la pembeni, watu wamesongamana madirishani na kila mahali, wamesimama kuzunguka kuta za Maskani. Haya basi. Nao wakasema, lilipozuka, watu wa hapa mjini, walisema, "Katika muda wa miezi sita . . . " Sisi tukiwa na dola moja na senti themanini za kujenga Maskani, watu wengi wa gereji tayari walikuwa wameamua itakuwa gereji yao. Lakini ingali ni zizi la kondoo kwa ajili ya Kondoo wa Mungu.

146 Moja, mbili, tatu, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. C, sita, saba, nane, tisa, kumi. Sawa.

147 Sasa, "Mimi Bwana nimeupanda, nitautia maji usiku na mchana wasije wengine wakaupokonya kutoka kwenye mkono Wangu." Angalia upinzani! Hakuna madhehebu ya kuliunga Hilo mkono. Hakuna makanisa yanayolipenda humu nchini. Hakuna Mpentekoste nchini, hakuna kitu kingine cha kulisaidia. Kila mtu anapinga ubatizo wa maji, kila mtu anapinga mambo haya mengine yote. Hata jamaa yangu mwenyewe, baba yangu mwenyewe alinifukuza nyumbani, nikaweka nguo zangu kwenye kijifuko cha karatasi nikaenda kuishi New Albany. Sawa.

> Lakini kupitia hatari nyingi, kazi ngumu na mitego,
> Nimekuja tayari;
> Neema ndiyo iliyonileta salama umbali huu,

Mimi nina umri wa miaka hamsini na sita, na hivi karibuni sina budi kuvuka ule mto.

> Neema itanipeleka mbele.

> Nitakapokuwa kule miaka elfu kumi,
> Niking'aa sana kama jua;
> Hatutakuwa na siku chache za kuimba sifa ya Mungu
> Kuliko tulipoanza kwanza.

Loo! jinsi ninavyompenda Yesu! Yeye ni kila kitu kwangu!

148 Loo, vema, ni wangapi nilioninii . . . Niliachia wapi, kumi? Tunaweza kuchukua wengine zaidi? Vema. Hiyo ilikuwa ni ya ngapi, kumi, kumi na tano? Vema. C, kumi mpaka kumi na

tano, po pote mlipo, kama mnaweza kusimama na kuingia. Ati nini? A-ha? Vema. C, kumi na tano hadi ishirini, basi. Hebu hiyo iwe ni C, kumi na tano hadi ishirini. Hiyo ingekuwa watu kumi zaidi. Tunaona . . . Mnaona—mnaona mahali mstari uliposimama pale, tusiwafanye—tusiwafanye wasongamane. Nasi tutaninii . . . Vema.

149 Sasa nisikilizeni kwa makini kabisa; hatutachukua muda mrefu. Lakini, sasa, loo! ni saa ya namna gani, ni wakati wa namna gani! La—laiti kila mtu angeweza kumpenda Bwana. Laiti—laiti sote tungefikia kile kiwango kutambua uwezekano wa dakika hii. Hebu tujaribu. Nisikilizeni tu kwa makini.

150 Tuna—tunajaribu kufanya kitu gani hapa? Tunalipitisha Neno la Mungu katika jaribio. Eliya alifanya jambo lile lile, akatoka akaenda mlimani baada ya yeye kujua ametumwa na Mungu kufanya jambo hilo. Yeye alisema, "Sasa hebu tuthibitishe nani ni Mungu, na Mungu yule ajibuye kwa moto na awe ndiye Mungu."

151 Nao hao makafiri wakajikatakata, loo! kasema, "Vema, hakika, hakuna . . ." Hao—hao makafiri walijua moto hautashuka, kwa hiyo wao wakapaza sauti na kupiga makelele.

152 Lakini Eliya alijua utashuka, maana yeye aliona ono kutoka kwa Bwana.

Unasema, "Ati aliona ono?"

153 Naam, bwana! Wakati alipoweka kila kitu katika utaratibu, alisema, "Bwana, nimefanya mambo haya yote kwa neno lako." Ndipo moto ukaanza kushuka. Wakati Neno la Mungu linatekelezwa kulingana na maandiko, basi ni kazi ya Mungu kushughulikia yaliyosalia. Yeye anakuomba tu uweke yote pale. Nawe hakikisha ya kwamba umeitwa kuyaweka pale. Mnaona? Na kama umeitwa, Yeye atashughulikia mengine.

154 Sasa, hapa kutakuweko na watu watakaopitia kwenye mstari huu nitakaokuwa ninawaombea . . . Sasa, vema, karibu mfikie ukutani sasa, vema, mstari uanze. Sasa, kwanza, angalau mahali fulani hapa jengoni, watu wengine . . .

Ni wangapi hapa walio wagonjwa nao hawana kadi ya maombi, inueni mikono yenu. Mnaona, kila mahali tu. Sasa, mnajua kama Bwana wetu . . . Nami ninaamini atafanya jambo hilo, iwapo Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye alifanya mistari ya maombi. Watu walimjia katika mistari mikubwa, halaiki ya watu, Yeye akawagusa, akawabariki. Halafu akasimama wakati mwingine na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Akaangalia kila mahali, akamwambia mwanamke sababu ya kumgusa Yeye; na akasema ugonjwa wake wa kutoka damu umekwisha, imani yake ilimponya.

155 Vipi kama angaligeuka akasema, “Vema, sijui, Bwana, nimekuwa na jambo hili kwa muda mrefu”? Haingetendeka. La, haingetendeka. La.

156 Vipi kama Yeye angalimwambia yule mwanamke Msirofoinike, “Kwa sababu ya neno hili ulilosema, binti yako, ibilisi amemtoka,” vipi kama angalisema, “Vema, sasa, Bwana, ni—nilikutaka ufanye jambo hilo namna *hii*”? I—iblisi bado angalikuwa ndani ya msichana yule. Bali yeye alitarajia kumkuta mtoto wake jinsi Yeye alivyosema angemkuta.

157 Sasa, Yeye alitwambia, “Kama unaweza kuamini! Kama unaweza kuuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, ila uamini kwamba hayo usemayo yatatukia, yatakuwa yako. Unapoomba, amini ya kwamba umeyapokea, nawe utapewa.” Ni ahadi ya namna gani!

158 Sasa mtu anayehubiri Injili ya kirafiki haamini jambo hilo kamwe. Yeye angeenda mlangoni, achungulie ndani, ama asimame pale, na kusema, “Vema, ni kundi lingine tu la watakatifu wanaojifingirisha,” na kuondoka. Mnaona? Lakini yeye hajui ya kwamba hiki ni Chakula kilichofichwa. Hajui ya kwamba hiki ni kile Kitu cha siri alichofichwa yeye. Hajui jambo hilo. Ni—ni—ni huzuni, mtu ambaye ni uchi, mwenye mashaka, kipofu, wala hajui. Mnaona? Hilo ni jambo baya.

159 Ee Mungu, hebu nife kwanza, lakini kamwe usinifanye namna hiyo. Afadhali nife (naam, bwana) kuliko kufanya jambo hilo. Nami nafikiri kila mmoja wetu angetaka hivyo, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

160 Lakini, sasa, Mungu ametuahidi mambo haya katika siku za mwisho. Katika Malaki 4, ilisema ya kwamba Yesu Kristo angeshuka na kujificha Mwenyewe nyuma ya ngozi ya mwanadamu kama alivyofanya huko Sodoma. Hiyo ni kweli. Naye alisema ya kwamba ulimwengu ungekuwa katika hali ya Sodoma. Na akasema, “Kama ilivyokuwa wakati huo, Mwana wa Adamu atafunuliwa siku hiyo.” Mnaona, huyu Mtu aliyeshuka katika namna ya mwanadamu, ambaye alikuwa “Elohimu,” kwa Ibrahimu, kabla ya huyu mwana wa ahadi kuja. Angalia ilikuwa nini, Ibrahimu alisema ilikuwa ni Mungu. Na Biblia ilisema watu watatu walimjia, mavumbi kwenye nguo zao, wamesafiri, wakaketi chini wakala kama wanadamu. Naye Yesu alisema, “Kwenye wakati uo huo ulimwengu utakapoingia katika hali ya Sodoma, ndipo Mwana wa Adamu atakapojifunua tena,” si Mwana wa Mungu. Mwana wa Adamu, unaona, angejifunua Mwenyewe.

161 Sasa linganisha jambo hilo na yale aliyosema nabii wa mwisho, “Angalieni, ninawapelekea Eliya nabii, naye ataigeuza mi—mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.” Mnaona? Ujumbe wa kuwarudisha kwenye Biblia, naye Mwana wa Adamu atakuwa akijifunua Mwenyewe katika siku hiyo. Na kwenye siku hiyo

ya sauti ya wakati wa mwisho wa kanisa, malaika wa saba, siri za Mungu zinapaswa kujulikana katika siku hiyo. Zile Muhuri Saba zingevunjwa. Siri za makanisa haya yote na kadhalika, jinsi yalivyotukia, na yale yaliyote-. . . jinsi, ni kitu gani kimetukia.

162 Mnaona, wao hawajui jambo Hilo. Yesu alisema, "Enyi Mafarisayo vipofu!" Kasema, "Kipofu akimwongoza kipofu, si wote wawili wataangukia shimoni?" Mnaona, hiyo ndiyo sababu watu hao hawaoni jambo Hilo.

163 Siri ya jambo Hilo, ni, zile Muhuri, kila moja ya makanisa hayo yalifanya madhehebu na kujiunga nayo, na hayo ndiyo moja ya mambo ya siri ambayo yamekuwa mabaya mbele za Mungu. Unaona hilo, Daktari Lee? Angalia, tazama. Ndivyo ilivyo. Hilo ndilo jambo lenyewe hasa hapo. Hiyo ndiyo moja ya zile siri. Wao waliunda madhehebu na, mnaona, nao wakatoka kabisa nje ya mapenzi ya Mungu. Na jambo hilo litaanikwa hadharani katika siku za mwisho, na kuwaongoza watu, si kwenye kanuni ya imani wala madhehebu, bali kurudi kwenye Neno la kweli. Na hilo Neno la kweli litalijia kundi fulani la watu, na Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe katikati yao, "yeye yule jana, leo, na hata milele."

164 Loo, jamani! Loo, ninapenda jambo hilo. Ninapenda—ninapenda kujivunia Yeye. Ninapenda ku—kumfanya Yeye mkubwa mbele za watu. Hainilazimu kumfanya mkubwa; Yeye tayari ni mkubwa. Yeye yuko juu sana huwezi kumruka, ni wa kina sana huwezi kufika chini Yake, ni mpana sana huwezi kumzunguka, lakini hata hivyo una nafasi moyoni mwako kwa ajili Yake. Je! hutampokea? Jinsi Bwana wetu alivyo wa ajabu! Vema.

165 Sasa hebu tunyamaze kimya kabisa, kila mtu. Sasa, tumezungumza juu ya jambo Hili. Na sasa swala lenyewe, ni, je! jambo Hilo ni kweli? Sasa, huenda kukawa na wageni hapa. Huenda nikasema kama. . .kwenu, kama Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye angefanya nini katika dakika hii? Angefanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa hapo awali. Hiyo ni kweli? Imani ya watu ingegusa vazi Lake, Naye angegeuka. Kama alivyomfanyia yule mwanamke pale kisimani, na aliyofanya mahali pengine, Naye aliyatambua mawazo yao.

Sasa, unasema, "Yeye angeweza kuniponya?"

166 Neno Lake lilisema Yeye tayari amefanya jambo hilo. Lakini jambo lenyewe ni, ni, kujifunua kwamba Yeye yuko hapa.

167 Sasa, kama Yeye angalitutokea katika mwili wa kawaida, akionekana kabisa kama picha ya Hofmann iitwayo *Kichwa cha Kristo Akiwa na Miaka Thelathini na Mitatu*, na damu ikitiririka kutoka kwenye mkono Wake, na kadhalika, amejaa makovu ya misumari, mimi sigelikubali jambo hilo. La, la. La, la. Atakapokuja, Yeye Mwenyewe, "Kila jicho litamwona,

kila ulimi utamkiri Yeye; na kama vile umeme unavyotoka Mashariki ukaenda Magharibi, ndivyo itakavyokuwa." Mnaona? Hatuamini madhehebu haya na vikundi vya dini. Tunaamini Mungu ni Neno.

168 Lakini Yeye huvaa mwili, anachukua mwili wako na mwili wangu, na anawapa vipawa, ananipa vipawa, na kupitia vipawa hivi Yeye anajitambulisha. Hicho ndicho Chakula cha siri. Haidhuru atajitambulisha kwangu kiasi gani, hamna budi kuamini jambo Hilo, hamna budi kuwa na kipawa cha imani, pia, kuamini jambo Hilo. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Na sasa kama Yeye atajidhihirisha Mwenyewe kwa njia hiyo, je! mtamwamini Yeye? ["Amina."] Kwa moyo wenu wote, mtamwamini? Loo! ni ajabu jinsi gani, namngojea Yeye tu, nangoja tu kuona atakalosema.

169 Hapa yupo mtu anayesimama hapa. Sijapata kumwona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Anaonekana kama ni mtu mzuri, na mwenye nguvu, na mwenye afya, na labda ndivyo alivyo, si—si—sijui. Lakini yeye anasimama pale. Sasa, ningeweza kwenda niweke mikono juu ya mtu huyo na kumwombea, nimwulize kama angeamini. Yeye angeweza kusimama hapa na kuniambia, aseme, "Mimi—mimi—mimi nataka umwombee *Fulani*. Nami nina—nina maumivu mabaya. Ninaumwa na kichwa, kila wakati. Nina vidonda vya tumbo," ama kitu fulani. Yeye—yeye, sijui. Yeye angeweza kusema moja ya mambo hayo.

170 Ningesema, "Vema, bwana, ndugu. Nitaweka mikono yangu juu yako na kukuombea." Hilo lingekuwa sawa kabisa. Hivyo ndivyo tulivyofanya hasa katika nyakati zote. Hilo ni kweli?

171 Lakini, kumbukeni, Yesu alisema ingekuwa vinginevyo karibu tu na Kuja Kwake, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Na yule Mtu aliyekuja, alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema alimokuwemo Sara, Naye akasema, (si "Abramu," sasa) "Ibrahimu."

172 Mnaona, yeye alikuwa Abramu, jana yake. Lakini alikutana na ono, na Bwana akamwambia ya kwamba, "Nitabadilisha jina lako."

173 Naye Bwana yuko hapa, Mwenyewe, katika umbo la mwanadamu, akila na kunywa pamoja naye. Kasema, "Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sara?" S-a-r . . . r-a-i; sio S-a-r-a.

Akasema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

174 Kasema, "Nitakuzuru, kulingana na ahadi Yangu miaka ishirini na mitano iliyopita."

175 Naye Sara kwa namna fulani akijichekea. Akasema, "Sara amecheka hemani sasa hivi, akisema, 'Mambo haya yawezekanaje?'" Kuna neno lililo gumu la kumshinda Mungu? Mnaona? Hakuna. La, bwana.

176 Sasa Yeye alisema, Yesu aliahidi ya kwamba, "Yeye, Mwana wa Adamu," ambaye ni Neno, (mnaamini jambo hilo?) "angekuja katika siku za mwisho na angejifunua Mwenyewe katika ule wakati ambapo ulimwengu ungekuwa kama Sodoma na Gomora." Mnaamini jambo hilo ni kweli?

177 Kabla hatujaomba ombi moja, baadhi yenu huko nje ombeni mwone kama Mwana wa Adamu yungali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wewe omba tu kama Yeye ndivyo alivyo, useme, "Bwana, mtu huyu hanijui mimi, lakini ninajua ya kwamba ni wewe yule jana, leo, na hata milele," uone kama atakwambia jambo hilo.

Ndiyo, bwana. Sasa inua kichwa chako kwa muda kidogo tu.

178 Yuko nyuma yangu. Ni mtoto. Ana joto kali sana la homa sasa hivi. Ni msichana mdogo. Umetoka nje ya mji. Mtoto huyo ana ugonjwa wa tumbo. Alikuwa nao. Amini tu.

179 Sasa, hivyo ndivyo alivyosema Yeye angefanya? Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu. Mungu Mbinguni anajua jambo hilo.

180 Mtu huyu hapa, yeye anaonekana ana nguvu sana na ni mwenye afya. Lakini mnaona kile kivuli juu yake pale? Hiyo ina maana kwamba, Mungu asipomsaidia, yeye hatakuwa hapa muda mrefu sana. Yeye ana kansa. Iko ndani ya pafu lako.

Sasa, Mwana wa Adamu yuko hapa.

Ana mzigo moyoni mwake kwa ajili ya mvulana mdogo, mtoto mdogo. Hiyo ni kweli? Unaamini Mungu anaweza kuniambia mtoto huyo ana kasoro gani? [Huyu ndugu anasema, "Ninajua anaweza."—Mh.] Anaweza. Yeye huzimia kidogo kama namna fulani ya kifafa. Ndiyo kwanza azimie hivi majuzi. ["Asubuhi ya leo."] Hiyo ni kweli, asubuhi ya leo. Nawe unaamini utaishi upate kumlea mvulana huyo, naye atakuwa na afya? ["Naam."]

181 Yuko wapi Charlie Cox? Yuko wapi? Charlie, uko wapi? Nilifikiri alikuwa hapa usiku wa leo. Hapa, Charlie. Gary, uko wapi, Larry, yeye yuko hapa? Mvulana wake mdogo alikuwa na kitu kile kile, kitu kile kile kabisa. Uko wapi, Larry? Njoo hapa kidogo. Vema, umefika. Mvulana huyu mdogo hapa alikuwa na jambo lile lile. Baba yake na mama yake ni marafiki wangu sana. Miaka mingi iliyopita nilikuwa kule, naye huyu mvulana mdogo angeshikwa na kifafa, amezimia tu kudhoofika. Kilikuwa kifafa. Nilikipata kwa mvulana huyo mdogo, nikamwomba Mungu amponye. Yeye hajashikwa nacho tangu wakati huo. Yule ni baba yake; mama yake ameketi mahali fulani hapa; na yuko hapa huyo mvulana mdogo, mwenyewe.

182 Sasa unaamini, bwana? (Asante, Larry.) Unaamini, bwana? Mungu wa Mbinguni na akujalie jambo lile lile, na wewe uishi upate kumlea mtoto yule. Mungu akubariki.

Na tuombe.

183 Mungu mpendwa, msaidie. Ninaomba ya kwamba rehema Zako na neema ziwe juu yake na umbariki. Katika Jina la Yesu.

184 Rudi Louisiana sasa, mwenye furaha, ukimsifu Mungu kwa ajili yake.

185 Loo, naam, yeye alitoka Louisiana, hakika ndiko alikotoka, karibu na Ziwa Charles. Hakika. Mnaona, ninaweza kushika mawazo yako sasa. Mungu asifiwe!

186 Vema, unaomba ja—jambo jema, unataka kupata mtoto. Tayari ulikuwa na watoto, watoto kadha, lakini unataka mwingine. Mungu wa Mbinguni na akujalie jambo hilo, dada yangu. Njoo hapa, ninataka tu kukuwekea mikono.

187 Mungu mpenzi, mpe mwanamke huyu haja ya moyo wake, kwa sababu ni jambo linalostahili. Katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa nenda zako ukapate mtoto.

188 Mungu ni Mungu mwema. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Yeye anajua yote tuliyo na haja nayo. Yeye hutimiza haja zetu zote kama tukiamini. Alisema, "Kama unaweza kuamini!"

189 Nilikupa mkono mahali fulani. Sikumbuki ilikuwa ni wapi, lakini nilikupa mkono mahali fulani. Sikumbuki sawasawa, lakini tulikuwa mahali fulani, leo mahali fulani tu, lakini sijui ilikuwa ni wapi. Lakini hapo sipo, hatupo hapa kuzungumzia habari hizo. Uko hapa kuzungumza juu ya ninii, ama kuomba, unanitaka nimwombee mtu fulani mwingine. Hiyo ni kweli. Hayuko hapa. Yuko Georgia, mgonjwa. Si mgonjwa tu, kimwili, lakini kiroho yeye ni mgonjwa; binamu yako. Unaamini Mungu atashughulikia jambo hili kwa sababu umemtetea? Unaamini? Njoo hapa tuombe pamoja.

190 Mungu mpenzi, mjalie mtu huyu shauku ya moyo wake, apate kwenda na kumkuta mtu huyu akimlilia Mungu. Katika Jina la Yesu naomba. Amina.

Mungu akubariki. Usitilie shaka. Amini kwa moyo wako wote.

191 U hali gani? Si kwamba sikuushika mkono wako kukupa mkono wakati huo, ulipounyosha mkono wako, nilikuwa ninaona kitu fulani. Ilikuwa ni kivuli, cha giza hasa na cheusi. Hiyo ndiyo sababu. Najua nilishika mkono wako, nikakuta ni kweli, unaona. Lakini ni kansa. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuitoa? Iko kwenye titi lako, upande wa kushoto. Unataka kurudi Carolina na kumsifu Bwana kwa kuwa mzima, sivyo? Unaona ninalomaanisha? Na tuombe.

192 Mungu mpenzi, katika Jina la Yesu Kristo, Yeye aliyepo sasa; watoto wakila Chakula cha Mungu, jalia mtoto huyu pia afurahie imani, Chakula cha Mungu anachompa sasa kwa ajili

ya kuponywa kwake. Jalia aende na apate afya, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu. Amini kwa moyo wako wote.

U hali gani?

193 Je! huu si ni wakati mzuri sana? Inaonekana kama kwamba hofu iko juu ya watu hawa. Ama, inaweza kusikika kama, masikio yangu, kama tu kitu kinachosema, [Ndugu Branham anapulizia kwenye maikrofoni—Mh.] "Whii!" Kutoa sauti tu, kama, "Whii," namna hiyo, mnaona. Ni Chakula cha watoto. Mnaona? Ni chenu, Hicho ni kwa ajili yenu. Si kwa ajili yangu; ni kwa ajili yenu. Nina shukuru sana, kwenye wakati uu huu sasa, sininii . . . Mimi ni mzima, nijuavyo mimi; lakini ni Hicho ni chakula kwa ajili yangu, pia, ninapokihitaji. Ni Chakula kwa ajili yenu. Ni kutia moyo. Kwenu ambao hata si wagonjwa, linaleta tu mioyo yetu mbele za Mungu.

194 Hiki kiko katika wakati wake kabisa, yale aliyosema Yeye angefanya, "Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa." Mnaona? "Na, tazama, ninawapelekea Eliya nabii kabla haijaja siku ile ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya. Yeye atairejeza mioyo ya watu kuelekea Baba zao." Mnaona? Mnaona?

195 "Halafu wenye haki watatembea juu ya wa—waovu, majivu." Watateketea kama tanuru, mnaona, dunia itateketea. Tunaona itaanguka kule ng'ambo. Na volkeno itasambaa duniani, na mbingu zitawaka moto.

Ee Mwamba wenye imara, nirehemu sasa, na wakati huo.

196 U hali gani? Vema, jambo moja, una ugonjwa wa mabibi, shida ya wanawake. Una mambo mengine. Wewe una wasiwasi, uko kwenye umri ule tu wa kushikwa na wasiwasi. Maradhi ya kila namna. Lakini una haja, pia, hiyo ni kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyo. Unaamini ya kwamba una ninii . . . Umetubia kila kitu? Unaamini nikikuwekea mikono na kumwomba Mungu afanye jambo hilo, Roho Mtakatifu atakuja? [Dada anasema, "Ndio."—Mh.] Unaamini jambo hilo? ["Ndiyo, bwana."] Na tuombe.

197 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu, katika namna ya kimitume, na kuomba ya kwamba apokee ubatizo wa Roho Mtakatifu. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba aupokee. Amina.

198 Usilionee shaka. Ni wako, unaona. Ni wako. Ni Cha—Chakula cha watoto.

199 Ulisikia kitu fulani kigeni niliposema, "ugonjwa wa wanawake," sivyo? Maana huo ndio uliokuwa nao, pia. Sasa unaamini utakuwa mzima sasa hivi? Nenda zako, ukimshukuru tu Bwana.

200 U hali gani? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini utaweza kula kama ulivyokuwa unakula muda mrefu uliopita? Vema. Nenda zako, na useme, "Asante, Bwana. Ninaamini hilo." Uwepo wa Bwana.

201 Unaamini ugonjwa huo wa mgongo utakuacha na utakuwa mzima? Vema, nenda zako, ukisema, "Asante, Mungu mpenzi," na Mungu atakujalia.

202 Unaamini unaweza kuwa mzima, Bwana atakupa afya; wala hutakuwa na yabisi kavu, utakuwa mzima na mwenye afya? Unaamini jambo hilo? Nenda zako, ukimshukuru Yeye, sema, "Bwana, ninakubali kwa moyo wangu wote, na ninaamini jambo Hilo."

Ninyi nyote mlio huko nje mnaamini nini juu Yake?

203 Wewe uliye papa hapa, weka mkono wako juu ya huyo mwanamke aliyeketi karibu sana nawe pale, umwambie mishipa ya damu iliyovimba na yabisi kavu itamwacha. Wakati ataninii . . .?. . .

204 Mungu akubariki. Unaamini utapona sasa. Nenda zako nyumbani na uwe . . . Mungu akubariki. Nenda zako, na useme, "Asante, Bwana Yesu."

205 U hali gani? [Dada anasema, "Bwana asifiwe."—Mh.] Unaamini ugonjwa huo wa wanawake utakuacha, pia? ["Ninaamini."] Nawe utapata afya? ["Asante, Yesu."] Nenda zako, na useme, "Asante, Bwana." ["Asante, Yesu."]

206 U hali gani? [Dada anasema, "Mfupa mwororo uliopasuka."—Mh.] Mbona, jamani, jamani! ["Totten"] Ninajua jina lako. Ni—nilikuwa nikininii . . . ["Totten."] nilipokuwa mchungaji wa kanisa la Kibatisti. ["Totten."] Totten. ["Della Totten."] Dada Della Totten. Una ugonjwa wa mgongo sasa. ["Ndio."] Utapona. Unaamini Yeye atakuponya? ["Ndio."] Unakumbuka yaliyotukia kule kwenye kanisa la Kibatisti la Milltown miaka mingi iliyopita? ["Ndio, ninakumbuka hayo!"] Yeye angali ni Mungu yeye yule leo. ["Loo! asante Mungu!"] Mungu akubariki, dada yangu.

George Wright, uko wapi? Unakumbuka? Jamani, jinsi . . .

Unaamini, kama niliweka tu mikono yangu juu yako, nikiwa na upako huu, unaamini utapata afya? Njoo hapa. Katika Jina la Yesu Kristo na aponywe. Amina. Uwe na imani!

Vema, nyote mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

207 Sasa, jinsi jambo hilo linavyoleta kumbukumbu za kale, kumwona bibi huyo! Siwezi kukumbuka jina lake, bado, lakini mimi . . . [Mtu fulani anasema, "Totten."] Totten. Totten, hiyo ni kweli. Loo, naam, binti yake alikuwa Birdie, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Msidhani nimerukwa na akili, mimi kwa namna

fulani kidogo tu ninaninii, mwajua, kwa namna fulani nininii . . . siwezi kueleza jambo hilo.

208 Lakini ugonjwa wako wa mgongo umekwisha, bibi. Nenda, ukamsifu Bwana, na kusema, "Asante, Bwana."

209 Unaamini ugonjwa wako wa mgongo utapona, pia? [Mgonjwa anasema, "Naam."—Mh.] Nenda zako tu, ukafurahi, na kusema, "Asante, Bwana Yesu," na uamini Hilo. Vema. Uwe na imani sasa. Usione shaka.

210 Njoo, bibi. Unaamini kwa moyo wako wote? Una kasoro nyingi. Una ugonjwa wa mgongo, pia. Unaamini Mungu atakuponya? Vema, nenda tu, ukifurahi. Huyo, huyo ni Yeye anayekufanya ujisikie namna hiyo. Mshukuru Bwana. Mungu akubariki, dada.

211 Habari, mwanangu. [Mvulana anasema, "Njema!"—Mh.] Unaamini ya kwamba Mungu ataponya wasiwasi wa yule mtoto na kumpa afya? Unaamini hilo? Vema. Habari, rafiki mpenzi, hebu nikupe mkono.

212 Mungu mpenzi, ondoa kitu hicho kiovu kutoka kwa mvulana huyu mdogo, na jalia aishi na awe mtu wa kawaida. Katika Jina la Yesu. Amina.

213 Mungu akubariki, ndugu. Unaamini jambo hilo, sivyo? Na utapata afya. Usione shaka hata kidogo.

214 U mdogo mno kupata ugonjwa wa moyo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? [Huyo mgonjwa anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Nenda zako, ukaseme, "Asante, Bwana, kwa kuniponya."

215 Unaamini Mungu ataponya ugonjwa wa tumbo na kukupa afya? Nenda zako, ukafurahi, na kusema, "Asante, Bwana."

216 Yeye yungali Mungu, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Jambo likupasalo kufanya tu ni kuamini tu. Hiyo sio kweli? Unaamini Mwana wa Adamu katika siku za mwisho?

217 Kuna jambo lililotukia hapa dakika chache zilizopita, nami siwezi . . . ninajaribu kuona ilikuwa ni wapi. Mtu fulani alikuwa na imani na akafanya jambo fulani. Ama, labda nitawapata Jumapili ijayo, ama niwezapo. Wewe ni—ni . . . Hiyo hapo tena. Umeinua mkono wako. Unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa moyo, akupe afya, amponye binti yako pale mwenye—mwenye . . . Unaamini hilo? Bibi Neff, unaamini ya kwamba Mungu . . . Leo Neff. Sikujui, bali hilo ndilo jina lako. Una ugonjwa wa moyo, na binti yako mdogo ana ugonjwa wa figo. Unaamini atapona? Imani yako inakuponya. Amini kwa moyo wako wote.

218 Wewe uliye nyuma kule kwenye kidimbwi, unayesimama pale nyuma na ugonjwa wa tumbo, Yesu Kristo anakuponya.

219 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hebu na tuwekeane mikono yetu sisi kwa sisi sasa. Loo! wazieni juu ya saa tunayoishi, wazieni wakati huo. Wazieni ya kwamba tuko katika Uwepo halisi wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Yeye aliahidi angefanya jambo hili katika siku za mwisho. Nimeweka mikono juu ya hizi leso.

220 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utabariki hizi leso kwa ajili ya kuponywa kwa miili ya watu, katika Jina la Yesu Kristo.

221 Sasa, huku mikono yenu ikiwa juu ya mmoja kwa mwingine, kila mmoja wenu ni mshiriki wa Mwili wa Kristo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyeahidi kufunua siri za mioyo na kufanya mambo haya, Yeye yuko ndani yenu. Wewe ni sehemu Yake, Naye ni sehemu yako. Sasa, Yeye alisema hivi, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yaani wewe. “Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Sasa, usijiombee, mwombee yule uliyemwekea mikono, maana wao wanakuombea wewe. Sasa na tuombe pamoja, na kusiwe na mtu mnyonge ye yote kwenye hili jengo. Kwa nini tungojee tena zaidi, ndugu yangu mpendwa, dada, Huyu hapa, Roho Mtakatifu, Mungu, papa hapa, jambo lenyewe hasa tulilozungumzia.

222 Yesu mpenzi tunautambua Uwepo Wako. Ulimfufua yule mtoto mchanga kule nyuma juzijuzi, baada ya kufa, kwa maombi ya imani. Mungu mpenzi, kuna wengi hapa hatukuweza kuwafikia, wakati unapita, lakini wao wamewekeana mikono. Wao ni waamini. Tumeketi katika Uwepo wa Bwana Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu, yeye yule jana, leo, na hata milele.

223 Shetani, umeshindwa! Yesu Kristo alikushinda! Yeye alifufuka katika wafu na anasimama miongoni mwetu usiku wa leo, akithibitisha Ujumbe huu wa siku za mwisho. Toka katika watu hawa! Waache, katika Jina la Yesu Kristo! “Katika Jina Langu watatoa pepo,” nawe umetolewa nje. Katika Jina la Yesu Kristo, liache kusanyiko hili!

224 Kila mmoja wenu anayekubali kuponywa kwake, simama kwa miguu yako. Kila mmoja anayekubali kuponywa, simama kwa miguu yako. Inueni mikono yenu sasa na mumpe Yeye sifa!

“Sasa nakubali kuponywa kwangu,” mwambie Mungu jambo hilo, sasa nakubali kuponywa kwangu. [Kusanyiko linasema, “Sasa nakubali kuponywa kwangu.”—Mh.] Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Kristo. [“Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Kristo.”] Sasa ninakuamini. [“Sasa ninakuamini.”] Saidia kutokuamini kwangu.” [“Saidia kutokuamini kwangu.”] Amina. [“Amina.”]

Nitamsifu, nitamsifu,
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;

Mpeni Yeye utukufu, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

225 Je! hamumpendi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu tumsifu Yeye basi. Kila mtu, huku mmeinua mikono yenu juu, mpeni sifa, wakati ndugu anakuja hapa kuturuhusu tufumukane.

CHAKULA CHA KIROHO KWA WAKATI WAKE SWA65-0718E
(Spiritual Food In Due Season)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 18 Julai, 1965, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1999 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org